JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

TAASISI YA ELIMU TANZANIA

RASIMU

# RASIMU YA RIPOTI YA KAMATI YA KITAIFA YA WATAALAMU YA KUSIMAMIA KAZI YA MABORESHO YA MITAALA YA ELIMU YA AWALI, MSINGI, SEKONDARI NA UALIMU

Mei, 2023

# Yaliyomo

**Orodha ya Majedwali** ........ **vii**

**Orodha ya Vielelezo** ........ **viii**

**Vifupisho** ........ **ix**

**Shukurani** ........ **x**

**1.0 Utangulizi** ........ **1**

1.1 Hadidu za Rejea ........ 2

**2.0 Methodolojia** ........ **3**

**3.0 Maoni ya Wadau** ........ **4**

3.1 Ukusanyaji wa Maoni ........ 4

3.2 Matokeo ya Utafiti ........ 4

3.2.1 Elimu ya Awali ........ 5

3.2.2 Elimu ya Msingi ........ 5

3.2.3 Elimu ya Sekondari ........ 6

3.2.4 Elimu ya Ualimu ........ 7

3.2.5 Utekelezaji wa Elimu Jumuishi ........ 7

3.3 Hitimisho ........ 8

**4.0 Mapendekezo ya Mfumo wa Elimu** ........ **9**

**5.0 Muundo Pendekezwa wa Elimu** ........ **12**

5.1 Muundo wa Elimu ........ 12

5.2 Ufafanuzi wa Muundo ........ 15

5.2.1 Elimu ya Awali ........ 15

5.2.2 Elimu ya Msingi ........ 15

5.2.3 Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini ........ 16



Taarifa ya Kamati Final.indd 2 08/05/2023 15:04

RASIMU

5.2.4 Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu .............................. 22
5.3 Uthibiti Ubora .............................................................. 22

**6.0 Mapendekezo Kuhusu Mitaala.................................................... 23**
6.1 Dira na Malengo Makuu ya Elimu ........................................ 23
6.1.1 Dira ya Elimu ........................................................ 23
6.1.2 Malengo Makuu ya Elimu ......................................... 23
6.2 Malengo ya Elimu kwa Kila Ngazi ........................................ 24
6.2.1 Malengo ya Elimu ya Awali ....................................... 24
6.2.2 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la Kwanza hadi la Pili .................................... 24
6.2.3 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la Tatu hadi la Sita ........................................ 25
6.2.4 Malengo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini – Elimu ya Jumla .............................. 25
6.2.5 Malengo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini – Elimu ya Amali .............................. 26
6.2.6 Malengo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu ........... 27

**7.0 Umahiri wa Jumla na Masomo kwa Kila Hatua ya Elimu........... 28**
7.1 Utangulizi ........................................................................ 28
7.1.1 Kuwasiliana .......................................................... 28
7.1.2 Ubunifu, Fikra Tunduizi na Utatuzi wa Matatizo ....... 29
7.1.3 Ujuzi wa Kidijitali .................................................. 29
7.1.4 Kushirikiana na Uzalendo ........................................ 30
7.1.5 Wingi wa Maudhui .................................................. 30
7.1.6 Kuhakikisha Mtaala Unakidhi Mahitaji ..................... 32
7.2 Umahiri wa Jumla, Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ............ 32



Taarifa ya Kamati Final.indd 3 08/05/2023 15:04

7.2.1 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Awali........................ 33

7.2.1.1 Maeneo ya Ujifunzaji............................................... 33

7.2.2 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la Kwanza hadi la Pili .................................................... 34

7.2.2.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Umahiri Mkuu.................... 34

7.2.3 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la Tatu hadi la Sita ....................................................... 34

7.2.3.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Elimu ya Msingi Darasa la Tatu hadi la Sita............... 35

7.2.4 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini – Elimu ya Jumla.............................................. 36

7.2.4.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini – Elimu ya Jumla.............. 36

7.2.5 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini – Elimu ya Amali........................................ 37

7.2.5.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini – Elimu ya Amali.............. 38

7.2.6 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu ......................................................... 40

7.2.6.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu ............................................ 41

**8.0 Elimu ya Ualimu ......................................................................... 43**

8.1 Utangulizi ....................................................................... 43

8.2 Mifumo ya Uandaaji wa Walimu ............................................ 43

8.3 Mapendekezo ya Mfumo wa Elimu ya Ualimu Nchini Tanzania............................................................... 47



Taarifa ya Kamati Final.indd 4 08/05/2023 15:04

8.3.1 Mafunzo kwa Vitendo ........ 50

8.4 Weledi, Hadhi na Motisha kwa Walimu ........ 50

8.5 Mitaala ya Elimu ya Ualimu ........ 52

8.6 Malengo ya Elimu ya Ualimu ........ 54

8.6.1 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu ........ 54

8.6.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu ........ 54

8.7 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ualimu ........ 54

8.7.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Stashahada ya Ualimu ........ 55

8.8 Umahiri wa Jumla wa Astashahada ya Ukufunzi wa Karakana/ Maabara (Elimu ya Amali) ........ 57

8.8.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Astashahada ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara (Elimu ya Amali) ... 58

8.9 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 58

8.10 Upimaji na Tathmini ya Ujifunzaji na Ufundishaji ........ 59

**9.0 Mikakati ya Utekelezaji ........ 61**

9.1 Utangulizi ........ 61

9.2 Mikakati ya Utekelezaji wa Mitaala Mipya ........ 61

9.2.1. Utekelezaji Kuanza na Darasa Moja kwa Wakati Mmoja ........ 61

9.2.2. Utekelezaji katika Madarasa Yote kwa Pamoja ........ 62

9.2.3. Utekelezaji kwa Pamoja katika Makundi ya Madarasa ........ 62

9.2.4. Utekelezaji Kuanza na Darasa Moja Moja katika kila Kundi ........ 62

9.3 Mkakati Unaopendekezwa ........ 63


RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 5 08/05/2023 15:04

**10.0 Muhtasari wa Mapendekezo Makuu ... 66**

10.1 Muundo wa Elimu Rasmi ... 66

10.2 Mitaala ... 68

10.3 Elimu ya Ualimu ... 70

10.4 Utekelezaji ... 71

10.5 Sheria ... 71

**Marejeleo ... 72**

RASIMU

# Orodha ya Majedwali

**Jedwali Na. 1:** Muundo Pendekezwa wa Elimu ..................................... 13

**Jedwali Na. 2:** Maeneo ya Ujifunzaji na Umahiri Mkuu Elimu ya Awali..33

**Jedwali Na. 3:** Maeneo ya Ujifunzaji na Umahiri Mkuu Elimu ya Msingi Darasa la Kwanza hadi la Pili ............................. 34

**Jedwali Na. 4:** Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo Elimu ya Msingi Darasa la Tatu hadi la Sita .................................. 35

**Jedwali Na. 5:** Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini- Elimu ya Jumla..................................... 36

**Jedwali Na. 6:** Orodha ya Fani Mbalimbali za Elimu ya Amali - Sekondari Hatua ya Chini............................................... 38

**Jedwali Na. 7:** Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu .................................................. 41

**Jedwali Na. 8:** Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Stashahada ya Ualimu (Elimu ya Awali)......................... 55

**Jedwali Na. 9:** Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Stashahada ya Ualimu (Elimu ya Msingi)............................................. 56

**Jedwali Na. 10:** Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Stashahada ya Ualimu (Elimu Maalumu)............................................. 56

**Jedwali Na. 11:** Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Astashahada ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara (Elimu ya Amali)........ 58

**Jedwali Na. 12:** Mkakati wa Utekelezaji wa Mitaala Mipya kwa Makundi ya Madarasa.................................................................. 63

RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 7 08/05/2023 15:04

# Orodha ya Vielelezo

**Kielelezo Na. 1**: Muundo wa Elimu Uliopo ........................................... 10

**Kielelezo Na. 2:** Muundo Pendekezwa wa Elimu .................................. 14

**Kielelezo Na. 3:** Michepuo ya Fani Mbalimbali za Mkondo wa Elimu ya Amali........................................................... 17

**Kielelezo Na. 4:** Michepuo Mipya Inayopendekezwa ............................ 21

**Kielelezo Na. 5:** Muundo Pendekezwa wa Elimu ya Ualimu ................. 48

RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 8 08/05/2023 15:04

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| AZAKI | Asasi za Kiraia |
| BEST | *Basic Education Statistics in Tanzania* |
| ICS | *Information and Computer Studies* |
| KKK | Kusoma, Kuandika na Kuhesabu |
| LAT | Lugha ya Alama ya Tanzania |
| NACTVET | *National Council for Technical and Vocational Education and Training* |
| NVA | *National Vocational Award* |
| OECD | *Organisation for Economic Co-operation and Development* |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| PSLE | *Primary School Leaving Examination* |
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| TEZ | Taasisi ya Elimu Zanzibar |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| VETA | *Vocational Education and Training Authority* |
| VVU | Virusi vya Ukimwi |
| WEMA | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali - Zanzibar |
| WJJMM | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu |
| WyEST | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |

RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 9 08/05/2023 15:04

# Shukurani

Maandalizi ya Ripoti hii yamehusisha wadau wengi wakiwemo watu binafsi, taasisi na asasi mbalimbali. Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Uboreshaji Mitaala inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha upatikanaji wa Rasimu za Mitaala ya Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi, Sekondari na Ualimu. Aidha, Kamati inatoa shukurani kwa taasisi zote za umma na binafsi na watu binafsi walioshiriki kwa namna moja ama nyingine katika kufanikisha uwepo wa rasimu za mitaala. Taasisi na mashirika hayo ni pamoja na: Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar (WEMA), Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia (WyEST), Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu (WJJMM), vyuo vikuu, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Taasisi ya Elimu Zanzibar (TEZ), Bodi na Manejimenti za Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Tanzania (VETA), menejimeti na wakufunzi wa Taasisi ya Sayansi ya Karume, Chuo cha Amali Zanzibar, Baraza la Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi (NACTVET), Baraza la Mitihani Tanzania (BMT), Umoja wa Wakuu wa Shule za Sekondari, Umoja wa Wakuu wa Shule za Msingi, shule za msingi na sekondari, pamoja na vyuo vya ualimu.

Aidha, Kamati inashukuru mashirika wahisani walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kuhakikisha rasimu za mitaala zinakamilika. Mashirika hayo ni: UNICEF, UNESCO*, Room to Read, Right to Play, Data Vision, Plan International, Norwegian Refugees Council, Christian Social Services Commission (CSSC), Global Education Link,* UWEZO*, Hill Packaging Ltd., Teacher Education Support Project (TESP), Madrasa Early Childhood Programme – Zanzibar* na *Educate!-Rwanda*. Pia, shukurani ziende kwa wadau wote wa elimu walioshiriki kutoa maoni kuhusu uboreshaji wa mitaala.

Mwisho, shukurani za kipekee ziende kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) kwa kuwezesha utayarishaji wa rasimu za mitaala.

**Prof. Makenya A. Maboko**
**Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Uboreshaji wa Mitaala**



Taarifa ya Kamati Final.indd 10 08/05/2023 15:04

# 1.0 Utangulizi

Tarehe 6 Aprili 2021, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati akiwaapisha viongozi mbalimbali wa serikali aliowateua, alitoa agizo kwamba mitaala ya elimu yetu ni lazima ifanyiwe marekebisho makubwa. Lengo la marekebisho hayo ni kufanya elimu ya Tanzania iweze kuwajengea wahitimu ujuzi utakaowawezesha kujitegemea na kutumia vyema fursa zinazopatikana nchini; hususan kumudu maisha yao ya kila siku, kujiajiri au kuajiriwa. Aidha, tarehe 22 Aprili 2021 Mheshimiwa Rais, wakati akilihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alirudia kutoa agizo hilo.

Kutokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ilianza kukusanya maoni ya wadau kuhusu mitaala ili kubaini upungufu uliopo na kupendekeza maboresho stahiki. Katika utekelezaji wa jukumu hilo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Adolf Faustine Mkenda (Mb.), aliunda kamati ya kitaifa ya wataalamu ili kusimamia zoezi zima la uboreshaji wa mitaala. Kamati hiyo ilijumuisha wajumbe wafuatao:

(i) Prof. Makenya A. Maboko (Mwenyekiti),
(ii) Dkt. Jennifer Sesabo,
(iii) Prof. Abel Ishumi,
(iv) Prof. Gastor Mapunda,
(v) Prof. Issa Haji Ziddy,
(vi) Dkt. Calvin Swai,
(vii) Dkt. Wadrine Maro,
(viii) Dkt. Ibrahimu Nzima,
(ix) Dkt. Lucas Luhende Kija,
(x) Bi. Sharifa Majid, na
(xi) Bi. Leah Dotto.



Taarifa ya Kamati Final.indd 1 08/05/2023 15:04

Aidha, Kamati ilikuwa na Sekretarieti yenye wajumbe watatu wafuatao:

(i) Dkt. Aneth Komba (Katibu),

(ii) Dkt. Godson Lema, na

(iii) Bw. Faridu Mohamed Wakil.

Kamati ilimchagua Dkt. Jennifer Sesabo kuwa Makamu Mwenyekiti.

## 1.1 Hadidu za Rejea

Kamati ya wataalamu ilifanya kazi zake kwa kuzingatia hadidu za rejea zifuatazo:

(i) Kusimamia na kuhakikisha kuwa hatua zote za uboreshaji wa mitaala zimefuatwa.

(ii) Kufanya uchambuzi wa kina wa taarifa ya hali ilivyo sasa yaani *Situation Analysis Report* na namna ambavyo taarifa hii itatafsiriwa katika kuandaa mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu.

(iii) Kuandaa picha kubwa ya mitaala itakayotumiwa na wataalamu katika kazi ya kuandaa mitaala na mihtasari kwa ngazi husika.

(iv) Kufanya vikao vya kimkakati na viongozi mbalimbali wa Serikali, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) na kutoa taarifa juu ya mwenendo wa mabadiliko ya mitaala.

(v) Kushiriki katika mikutano ya wadau yenye lengo la kuwashirikisha wadau juu ya mitaala mipya ya elimu.

(vi) Kufanya kazi kwa karibu na sekretarieti inayoongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa TET katika utekelezaji wa hatua zote zilizoainishwa kwenye mpango kazi wa ukuzaji wa mitaala.

(vii) Kuandaa mkakati wa utekelezaji wa mitaala inayopendekezwa (Rolling-out Strategy).

(viii) Kufanya kazi yeyote itakayojitokeza yenye lengo la kuhakikisha kuwa serikali inaandaa mitaala inayojenga ujuzi.

RASIMU

# 2.0 Methodolojia

Kabla Kamati haijaanza kazi, TET ilikuwa imeshaanza mchakato wa kukusanya maoni ya wadau kuanzia Aprili 2021. Aidha, TET ilichakata maoni hayo na kuandaa ripoti ya hali ilivyo sasa yaani "*Situation Analysis Report*". Mwishoni mwa mwezi Machi 2022, Kamati ikishirikiana na wataalamu wengine walioteuliwa kutoka taasisi mbalimbali, ilichambua ripoti hiyo na kubainisha maoni ya wadau kuhusu upungufu uliomo katika mitaala na mfumo wa elimu ya Tanzania na mapendekezo yao juu ya maboresho yanayohitajika. Aidha, Kamati iliendelea kupokea maoni ya wadau mbalimbali wakiwemo wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, viongozi wa dini, wamiliki wa shule zisizokuwa za serikali, asasi zisizo za kiserikali, viongozi waandamizi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar (WEMA), Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu (WJJMM), WyEST, OR-TAMISEMI na Bodi na Menejimenti ya Mamlaka ya Elimu ya Ufundi Tanzania (VETA), Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar (VTA), Taasisi ya Sayansi ya Karume, Zanzibar, Kamati ya Mapitio ya Sera ya Elimu, Kamati ya kufanya mageuzi makubwa ya Elimu Zanzibar, Tume ya vyama vya ushirika, Wakufunzi vyuo vya ualimu, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Akademia ya Sayansi Tanzania.

Baada ya kuchakata maoni ya wadau, Kamati ilirejelea falsafa ya *Elimu ya Kujitegemea* ya mwaka 1967; *Sheria ya Elimu Na. 25* ya mwaka 1978 na *Sera ya Elimu na Mafunzo* ya mwaka 1995. Vilevile, Kamati ilirejelea *Sera ya Elimu na Mafunzo* ya mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023, *Kiunzi cha Taifa cha Mtaala wa Elimumsingi na Elimu ya Ualimu* cha mwaka 2019 na *Ripoti ya Mapendekezo ya Elimu Nchini Tanzania (Tume ya Makweta)* ya mwaka 1982. Aidha, Kamati ilizingatia mahitaji ya kijamii na kiuchumi ya sasa; na ilipitia matamko ya kisera na kisheria ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Kamati pia ilipitia machapisho yanayoonesha mifumo ya elimu ya nchi mbalimbali ikiwemo Zambia, Mauritius, Ghana, Kenya, Ufini, Singapore, Ureno, Ujerumani, China na Malaysia ili kupata uzoefu wao.

Baada ya kuchambua matakwa ya sera, sheria, maoni ya wadau, uzoefu kutoka nchi mbalimbali na kwa kuzingatia hali halisi nchini, Kamati ilipendekeza maboresho katika muundo wa elimu. Vilevile, Kamati ilipendekeza maboresho kadhaa katika mitaala kama inavyofafanuliwa katika Ripoti hii. Maboresho hayo yamezingatia hoja za wadau wa elimu na yanalenga kujenga umahiri ambao unahitajika katika karne ya 21 katika ngazi zote za elimu.



Taarifa ya Kamati Final.indd 3 08/05/2023 15:04

# 3.0 Maoni ya Wadau

## 3.1 Ukusanyaji wa Maoni

Kama ilivyoelezwa awali, zoezi la kuboresha mitaala lilitanguliwa na ukusanyaji wa maoni ya wadau kuhusu mitaala inayotumika sasa ili kubaini upungufu uliopo na kupendekeza maboresho yanayohitajika. Ukusanyaji wa maoni ulikuwa na malengo mahususi yafuatayo:

(i) Kutathmini malengo ya elimu kulingana na mahitaji ya sasa na ya baadae.

(ii) Kubaini umahiri unaotakiwa kujengwa katika kila ngazi ya elimu.

(iii) Kuainisha njia za ufundishaji, ujifunzaji na upimaji ili kuboresha utekelezaji wa mitaala ya elimu.

(iv) Kubaini mahitaji ya rasilimali katika utekelezaji wa mitaala.

(v) Kuainisha njia za kuandaa, kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mitaala.

(vi) Kutathmini utekelezaji wa Elimu Jumuishi kulingana na mahitaji ya sasa na ya baadae.

Aidha, ukusanyaji wa maoni ulitumia mbinu za kitafiti zifuatazo:

(i) Kukusanya data msingi kupitia mikutano ya wadau, hojaji, mahojiano na mijadala ya vikundi lengani. Maoni ya wadau yalikusanywa kutoka katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, maoni yalikusanywa kutoka makundi mbalimbali ikijumuisha viongozi wa wizara, mikoa, wilaya, kata na shule. Maoni pia yalikusanywa kutoka kwa wazazi, wanafunzi, waajiri, wataalamu wa elimu, wajumbe wa bodi za shule, wabunge, viongozi wa dini, pamoja na Asasi za Kiraia (AZAKI).

(ii) Kuchakata data zilizokusanywa kutoka kwa wadau.

(iii) Kuchambua sera, miongozo, sheria, pamoja na mifumo ya elimu ya nchi mbalimbali.

(iv) Kupendekeza maboresho katika muundo wa elimu ya awali, msingi, sekondari, ualimu na katika mitaala iliyopo.

## 3.2 Matokeo ya Utafiti

Baada ya kuchakata maoni yaliyotolewa na wadau mbalimbali, yafuatayo yalibainika katika kila ngazi ya elimu:



Taarifa ya Kamati Final.indd 4 08/05/2023 15:04

### 3.2.1 Elimu ya Awali

Kwa upande wa Elimu ya Awali, wadau wengi walikuwa na maoni yafuatayo:

(i) Malengo ya Elimu ya Awali ya sasa, yaani kumwandaa mtoto kwa ajili ya Elimu ya Msingi na kumjengea stadi za maisha na za awali za ujifunzaji, hayatofautiani sana na yale ya nchi nyingine.

(ii) Asilimia 93 ya wadau walipendekeza Kiswahili kibaki kuwa lugha ya kufundishia katika ngazi hii.

(iii) Kuwe na vituo vya malezi vinavyojitegemea kabla ya kuanza Elimu ya Awali (umri 2-3) na baada tu ya Elimu ya Malezi watoto wajiunge moja kwa moja na Elimu ya Awali wakiwa na umri wa miaka 4-5.

(iv) Muda wa kipindi cha darasa la awali uongezwe kutoka dakika 20 za sasa hadi dakika 30.

(v) Watoto waanze kujengewa mapema stadi za kujitegemea na kujiajiri kulingana na umri wao.

(vi) Watoto wafundishwe elimu ya dini, maadili na uzalendo kuanzia Elimu ya Awali.

(vii) Idara ya Uthibiti Ubora katika wizara husika iwe ni idara inayojitegemea na iajiri wathibiti ubora wenye taaluma ya Elimu ya Awali tu.

(viii) Shule za awali zitenganishwe na shule za msingi.

### 3.2.2 Elimu ya Msingi

Kwa upande wa Elimu ya Msingi, wadau wengi walipendekeza yafuatayo:

(i) Asilimia 32 ya wadau walipendekeza umri wa kuanza darasa la kwanza uwe miaka sita (6) badala ya saba (7) ya sasa ambayo ilipendekezwa na asilimia 30 ya wadau.

(ii) Asilimia 53 ya wadau walipendekeza muda wa elimu ya msingi ubakie miaka saba (7) wakati asilimia 40.7 walipendekeza muda huo upunguzwe hadi miaka sita (6).

(iii) Baadhi ya maudhui katika mitaala iliyopo yanajirudiarudia na/au hayana manufaa kwa wanafunzi.

(iv) Baadhi ya maudhui muhimu hayamo katika mitaala iliyopo na hivyo yaingizwe.

(v) Mitaala ijenge umahiri unaomwezesha mhitimu kujitegemea kwa kujiajiri au kuajiriwa.


Taarifa ya Kamati Final.indd 5 08/05/2023 15:04

(vi) Mfumo wa elimu uwe nyumbufu kwa kuweka njia rasmi mbadala (kama ufundi, kilimo, uvuvi, sanaa na michezo) za kuendelea na mafunzo badala ya watoto wote kutegemewa kujiunga na elimu ya sekondari mara baada ya kuhitimu Darasa la Saba.

(vii) Wanafunzi wa Darasa la Kwanza na la Pili wafudishwe Kusoma, Kuandika na Kuhesabu tu pamoja na stadi wezeshi ambazo ni afya, mazingira, sanaa na michezo, ili kuwapunguzia mzigo wa masomo.

(viii) Wanafunzi wa Darasa la Tatu hadi la Saba wafundishwe masomo yatakayowasaidia kujenga umahiri wa kujitegemea, kujiajiri, na kujiendeleza na elimu ya juu.

(ix) Asilimia 53 walipendekeza lugha ya kufundishia iwe Kiswahili wakati asilimia 28 walipendekeza Kiingereza na asilimia 19 walipendekeza matumizi ya lugha za kiasili.

(x) Kwa shule zinazotumia lugha ya Kiswahili, Kiingereza kifundishwe kama somo kuanzia darasa la kwanza na kwa shule zinazotumia Kiingereza, Kiswahili kifundishwe kama somo kuanzia Darasa la Kwanza.

(xi) Upimaji wa wanafunzi usiegemee kwenye nadharia pekee bali pia upime vitendo, na usitegemee mtihani wa mwisho tu.

(xii) Miundombinu ya shule iwe fikivu na rasilimali (walimu na vifaa vya ujifunzaji na ufundishaji) ziwepo za kutosha.

(xiii) Walimu na wakaguzi wa shule wapewe mafunzo endelevu (*continuous professional development*).

### 3.2.3 Elimu ya Sekondari

Kwa upande wa Elimu ya Sekondari, wadau wengi walipendekeza yafuatayo:

(i) Umri wa kuanza Kidato cha Kwanza uwe miaka 12 na ule wa kuanza Kidato cha Tano uwe miaka 16. Aidha, muda wa masomo ubaki miaka minne kwa Kidato cha Kwanza hadi cha Nne na miwili kwa Kidato cha Tano na Sita kama ilivyo sasa.

(ii) Elimu ya Kidato cha Kwanza hadi cha Nne inyumbuliwe katika mikondo ya taaluma na ufundi wa fani mbalimbali kama biashara, kilimo, ufundi, michezo, sanaa, ushonaji, upishi nk.

(iii) Lugha ya kufundishia iendelee kuwa Kiingereza (72% ya wadau).

(iv) Baadhi ya maudhui katika mitaala iliyopo yanajirudiarudia na/au hayana manufaa kwa wanafunzi.



Taarifa ya Kamati Final.indd 6 08/05/2023 15:04

(v) Baadhi ya maudhui muhimu hayamo katika mitaala iliyopo na hivyo yaingizwe.

(vi) Mitaala ijenge umahiri unaomwezesha mhitimu kujitegemea kwa kujiajiri au kuajiriwa.

### 3.2.4 Elimu ya Ualimu

Kwa upande wa Elimu ya Ualimu, wadau wengi walipendekeza:

(i) Mkufunzi awe na shahada ya uzamili katika elimu na uzoefu kazini usiopungua miaka miwili katika ngazi husika.

(ii) Elimu ilenge kujenga uwezo wa mwalimu tarajali katika ujuzi utakaowasaidia wanafunzi kukua kitaaluma, kimaadili na kifikra.

(iii) Mafunzo yajumuishe stadi zitakazowawezesha walimu tarajali kuwa na stadi za maisha (kama fikra tunduizi, ubunifu, ujasiriamali, mawasiliano, ushirikiano, maadili, sayansi na kompyuta) ambazo zitawapatia uwezo wa kujitegemea na kujiajiri.

(iv) Muda wa mafunzo kwa ngazi ya stashahada uwe miaka mitatu: miaka miwili ya mafunzo ya taaluma na mmoja wa mafunzo kwa vitendo shuleni.

(v) Baada ya kuhitimu, walimu tarajali wafanye kazi chini ya uangalizi (*internship*) kwa kipindi cha mwaka mmoja.

(vi) Mwalimu tarajali afundishwe katika lugha ambayo ataenda kuitumia kufundishia.

(vii) Ngazi ya astashahada iondolewe kwenye mfumo wa elimu ya ualimu nchini.

### 3.2.5 Utekelezaji wa Elimu Jumuishi

Kuhusu utekelezaji wa Elimu Jumuishi, wadau walipendekeza yafuatayo:

(i) Wanafunzi wenye mahitaji maalumu wawe na madarasa ya awali ya peke yao.

(ii) Kuna umuhimu wa kutambua wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika ngazi zote ili afua stahiki zitolewe kwa wakati na kwa ufanisi.

(iii) Mwongozo wa ufundishaji na ujifunzaji katika madarasa jumuishi ubainishe aina za ulemavu na zana zinazotumika kuwatambua.

(iv) Kuwapo na msaidizi wa mwalimu (kama mkalimani wa lugha ya alama) katika kila darasa la awali ili kurahisisha utekelezaji wa elimu jumuishi.



RASIMU

Taarifa ya Kamati Final.indd 7 08/05/2023 15:04

(v) Kuwe na miundombinu fikivu na vifaa stahiki vya kujifunzia vinavyoenda sambamba na mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu pamoja na mabadiliko na ukuaji wa teknolojia duniani.

(vi) Mtaala wa ualimu uboreshwe na uwe nyumbufu ili kutoa fursa ya urekebifu kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi wote kujifunza kulingana na mahitaji yao.

(vii) Walimu waliopo kazini wapewe mafunzo ili waweze kutumia njia jumuishi za ufundishaji na upimaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

## 3.3 Hitimisho

Uchambuzi wa maoni ya wadau unaonesha kwamba mapendekezo yao mengi yanaweza kutengwa katika sehemu kuu tatu:

(i) Mapendekezo ya kisera: Haya yanagusa masuala kama muundo wa elimu (idadi na muda wa ngazi mbalimbali), umri wa kuanza kila ngazi ya elimu na lugha ya kufundishia.

(ii) Mapendekezo yanayohusu mitaala: Haya yanajumuisha masuala ya aina za umahiri unaotakiwa kujengwa, maudhui yanayofundishwa na mfumo wa upimaji.

(iii) Mapendekezo ya kiutekelezaji: Mengi ya mapendekezo haya yamelenga kwenye elimu ya malezi, Elimu ya Awali na elimu ya ualimu. Vilevile, eneo hili linajumuisha mapendekezo yote yanayohusu miundombinu, vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji, rasilimali watu na fedha.

RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 8 08/05/2023 15:04

# 4.0 Mapendekezo ya Mfumo wa Elimu

Mfumo rasmi wa elimu unaotumika sasa umezingatia kwa kiasi kikubwa *Sera ya Elimu na Mafunzo* ya mwaka 1995. Kwa mujibu wa mfumo huo, mwanafunzi anajiunga na shule ya msingi akiwa na umri wa miaka saba (7), na elimu hiyo inadumu kwa miaka saba (7). Baada ya hapo, wanafunzi wanaofaulu mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi hujiunga na Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini kwa muda wa miaka minne (4) ikifuatiwa na miaka miwili (2) ya Sekondari Hatua ya Juu kwa wale wanaofaulu vizuri. Baada ya kuhitimu Darasa la Saba au Kidato cha Nne, wanafunzi ambao hawakufanikiwa kuendelea na masomo wanaweza kujiunga na elimu ya amali inayotolewa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) kwa mafunzo yasiyozidi miaka mitatu (3). Aidha, wahitimu wa vyuo vya VETA na wa Kidato cha Nne wenye ufaulu stahiki wanaweza kujiunga na mafunzo ya Ufundi Sanifu kwa muda usiozidi miaka mitatu (3) na kutunukiwa stashahada na Baraza la Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Ufundi Sanifu (NACTVET). Stashahada hiyo pia inaweza kuchukuliwa na wanafunzi waliohitimu Kidato cha Sita ambao hawakufanikiwa kujiunga na elimu ya juu. Muundo huu wa elimu umefafanuliwa katika Kielelezo Na.1.


Kulingana na mfumo huu, elimu ya chuo kikuu kwa ngazi ya shahada ya kwanza hudumu kwa muda unaoanzia miaka mitatu (3) hadi mitano (5) kutegemeana na fani anayosomea mwanafunzi. Kwa kutumia takwimu za *Basic Education Statistics in Tanzania* za mwaka 2021, takribani asilimia 70.5 ya wahitimu wa Darasa la Saba waliweza kujiunga na elimu ya sekondari. Aidha, asilimia 36.5 ya wahitimu wa Kidato cha Nne waliweza kujiunga na mafunzo ya Kidato cha Tano. Hii ina maana kwamba idadi kubwa ya wahitimu wa elimu ya msingi na wale wa Kidato cha Nne hawaendelei na masomo ya ngazi inayofuata ingawa elimu wanayopata haijawatayarisha vyema kushiriki katika ulimwengu wa kazi.

Mfumo huu wa elimu umejikita katika mtazamo kwamba kila kijana wa Kitanzania anayeanza darasa la kwanza anatakiwa aendelee na elimu hiyo hadi kufikia chuo kikuu. Kwa mtazamo wa jamii, mkengeuko wowote kutoka kwenye njia hii pekee unachukuliwa kama dalili ya mwanafunzi husika kushindwa (*any deviation from this narrow path is deemed a failure*). Lakini ukweli ni kwamba sio kila kijana ana nia wala uwezo wa kufuata njia hiyo tu. Aidha, hakuna nchi



Taarifa ya Kamati Final.indd 9 08/05/2023 15:04

yoyote duniani ambayo vijana wake wote wanapitia njia hiyo na hakuna uchumi wowote duniani unaoweza kuendeshwa kwa ufanisi na watu wenye umahiri unaopatikana kupitia vyuo vikuu tu. Matokeo ya mfumo huu ni kwamba vijana wengi wanakata tamaa na mfumo wa elimu ambao wanauona hauna tija kwao. Hii imesababisha baadhi yao kuishia Darasa la Saba, kuacha shule kabla ya kuhitimu au kupoteza ari ya kujifunza. Moja ya athari za hali hii ni kuwapo kwa kundi kubwa la vijana wanaojiingiza katika vitendo vya kihalifu wakiwa na umri mdogo kwa sababu wameacha shule au wamehitimu bila mfumo wa elimu kuwapa stadi za kuwawezesha kumudu maisha yao kwa kujiajiri au kuajiriwa. Aidha, hali hii inasababisha hasara kubwa kwa taifa kwa kuacha kundi kubwa la Watanzania ambao hawawezi kushiriki kikamilifu katika ulimwengu wa kazi.




**Kielelezo Na. 1:** *Muundo wa Elimu Uliopo*

Ili kukabiliana na changamoto hiyo, ni muhimu kumpa kila mwanafunzi wa Kitanzania elimu itakayomwezesha kuishi kama raia mwenye uelewa wa kawaida wa mazingira yanayomzunguka (*socially responsible citizen*). Aidha, elimu hiyo impatie ama nyenzo za kuweza kushiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi yetu kwa kufanya kazi (*socially useful citizen*) au imwandae kuendelea na ngazi inayofuata ya elimu. Kwa kuzingatia maoni ya wadau, Kamati imebaini kwamba njia rahisi ya kuondokana na changamoto zilizopo katika mfumo wetu wa elimu ni kupendekeza muundo nyumbufu wa elimu.



Taarifa ya Kamati Final.indd 10 08/05/2023 15:04

Ni dhahiri kwamba sanjari na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, wadau wengi wanapendekeza kwamba mfumo wetu wa elimu uwe nyumbufu ili kuweza kukidhi mahitaji ya wanafunzi wenye uwezo, vipaji, na malengo mbalimbali katika maisha yao. Mataifa mbalimbali duniani yakiwemo yaliyoendelea na yanayoendelea yana mifumo nyumbufu ya elimu inayowaruhusu wanafunzi kufuata mikondo tofauti baada ya kipindi fulani cha elimu ya lazima. Mifano ya mifumo hiyo inatumika nchini Zambia, Mauritius, Uturuki, China, Ghana, Kenya nk. Tofauti iliyopo katika nchi hizo ni katika hatua gani mfumo wa elimu hunyumbuliwa. Wakati China, Ghana, Zambia na Kenya unyumbufu unaanza baada ya miaka 9 ya elimu, nchini Mauritius unyumbufu unaanza baada ya miaka 11 na nchini Uturuki unaanza baada ya miaka 8. Nchi nyingine zimeonesha kuanza kwa unyumbufu kulingana na umri wa mwanafunzi. Katika nchi nyingi zilizoendelea ikiwemo Australia, Kanada, Ufini, Uingereza na Marekani unyumbufu unaanza kwa wanafunzi wenye umri wa miaka 16 (sawa na Kidato cha Nne kwa muundo wetu wa sasa), nchini Austria na Ujerumani unyumbufu unaanza kwa wanafunzi wenye miaka 10 (sawa na Darasa la Tano kwa muundo wetu wa sasa) wakati Ubelgiji na Uholanzi unyumbufu unaanza kwa wanafunzi wenye miaka 12 (sawa na Darasa la Saba kwa muundo wetu wa sasa).

Ni wazi kwamba hatua ambayo mifumo ya elimu inanyumbuliwa inategemea kwa kiasi kikubwa hali halisi ya kijamii na kiuchumi ya nchi husika. Kama lengo kuu la kunyumbua mfumo wa elimu ni kuwapatia wahitimu ambao hawataendelea na ngazi inayofuata ya elimu stadi zitakazowawezesha kushiriki katika ulimwengu wa kazi, ni vema unyumbufu ukaanza kabla ya wahitimu wengi kutoka katika mfumo rasmi wa elimu. Kwa upande wa Tanzania, wanafunzi wengi huondoka katika mfumo rasmi wa elimu baada ya Darasa la Saba na baada ya Kidato cha Nne. Kwa mfano takwimu za *Basic Education Statistics in Tanzania* (BEST) za mwaka 2021, zinaonesha kuwa mwaka 2019, takriban wahitimu 300,000 wa Darasa la Saba hawakuendelea na masomo ya sekondari na takriban wahitimu 143,800 wa Kidato cha Nne hawakuendelea na masomo ya Kidato cha Tano. Hii ina maana kwamba kwa mwaka huo tu takriban vijana 444,000 walitoka kwenye mfumo rasmi wa elimu bila kuwa na stadi za kuwawezesha kushiriki katika ulimwengu wa kazi. Kwa kuwa lengo kuu la kunyumbua mfumo wa elimu nchini Tanzania ni kulipatia kundi hili kubwa la wahitimu stadi zitakazowawezesha kushiriki katika ulimwengu wa kazi, ni vema unyumbufu katika mfumo ufanyike kabla ya mwanafunzi kuhitimu Kidato cha Nne.


Taarifa ya Kamati Final.indd 11 08/05/2023 15:04

# 5.0 Muundo Pendekezwa wa Elimu

## 5.1 Muundo wa Elimu

Ingawa wadau wengi walipendekeza muda wa kusoma Elimu ya Msingi uendelee kuwa miaka saba (7), Kamati inapendekeza muda wa miaka sita (6) ili kukidhi matakwa ya *Sera ya Elimu na Mafunzo* ya mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023. Aidha, Kamati inapendekeza umri wa kuanza Darasa la Kwanza uwe miaka sita (6). Mapendekezo haya yanaenda sanjari na maoni ya wadau pamoja na uzoefu kutoka nchi mbalimbali. Kulingana na matakwa ya *Sera ya Elimu na Mafunzo* ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023, inapendekezwa kwamba Elimu ya Msingi itanguliwe na mwaka mmoja wa Elimu ya Awali kwa watoto wenye umri wa miaka mitano (5). Vilevile, Kamati inapendekeza muda wa Elimu ya Sekondari uendelee kuwa miaka sita (6): minne (4) ya Sekondari Hatua ya Chini (Kidato cha Kwanza hadi cha Nne) na miwili (2) ya Sekondari Hatua ya Juu (Kidato cha Tano na Sita). Mapendekezo haya pia yapo sanjari na maoni ya wadau na matakwa ya *Sera ya Elimu na Mafunzo*, 2014 kama ilivyorekebishwa mwaka 2023.

Kama inavyoelekezwa na *Sera ya Elimu na Mafunzo* ya mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023, Kamati inapendekeza kwamba elimu ya lazima (*compulsory basic education*) itolewe kwa muda wa miaka kumi (10) na ijumuishe miaka sita (6) ya Elimu ya Msingi na miaka minne (4) ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini. Hii ina maana kwamba kila mwanafunzi atakayeanza Darasa la Kwanza ataendelea kubaki shuleni hadi Kidato cha Nne. Kwa sababu hiyo, hakutakuwa na mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi, badala yake kutakuwa na upimaji wa kitaifa wa Darasa la Sita (*Standard Six National Assessment*) kama ilivyo sasa kwa wanafunzi wa Darasa la Nne na Kidato cha Pili.

Ili kukidhi maoni ya wadau juu ya umuhimu wa kuwapatia wahitimu wa elimu ya lazima stadi zitakazowawezesha kushiriki katika ulimwengu wa kazi, Kamati inapendekeza kunyumbua elimu ya Sekondari Hatua ya Chini katika mikondo miwili, yaani Mkondo wa Elimu ya Jumla (*General Education*) na Mkondo wa Elimu ya Amali (*Vocational Education*). Mfumo wa elimu unaopendekezwa umeoneshwa katika Jedwali Na.1 na Kielelezo Na. 2.



Taarifa ya Kamati Final.indd 12 08/05/2023 15:04


**Jedwali Na. 1:** Muundo Pendekezwa wa Elimu

| Ngazi | Hatua | Darasa | Muda (Miaka) | Umri (Miaka) |
|---|---|---|---|---|
| **Elimu ya Awali** | Awali | Shule ya Awali | 1 | 5 |
| **Elimu ya Lazima** | Elimu ya Msingi | Darasa la Kwanza na la Pili | 2 | 6-7 |
| | | Darasa la Tatu hadi Darasa la Sita | 4 | 8-11 |
| | Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini | Mkondo wa Elimu ya Jumla | 4 | 12-15 |
| | | Mkondo wa Elimu ya Amali | 4 | 12-15 |
| **Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu** | Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu (Elimu ya Jumla) | Kidato cha Tano na cha Sita | 2 | 16-17 |
| **Elimu ya Amali** | Elimu ya Amali Sanifu | Elimu ya Stashahada ya Amali Sanifu | 3 | 16+ |
| **Elimu ya Juu** | Elimu ya Jumla ya Juu | Elimu ya Shahada ya Kwanza | 3+ | 18+ |
| | Elimu ya Amali ya Juu | Elimu ya Shahada ya Kwanza | 3+ | 19+ |

RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 13 08/05/2023 15:04




**Kielelezo Na. 2**: *Muundo Pendekezwa wa Elimu*

## 5.2 Ufafanuzi wa Muundo

Kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na.1 na Kielelezo Na. 2, Kamati inapendekeza muundo wa elimu wenye ngazi kuu nne kama inavyofafanuliwa katika sehemu zifuatazo:

### 5.2.1 Elimu ya Awali

Elimu ya Awali ni hatua ya mwanzo ya elimu yenye lengo la kuwaandaa vyema watoto kwa ajili ya kuanza Elimu ya Msingi. Kama ilivyoelekezwa na *Sera ya Elimu na Mafunzo* ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023, Kamati inapendekeza kwamba Elimu ya Awali itolewe kwa muda wa mwaka mmoja na ipokee watoto wenye umri wa miaka mitano (5). Kwa kuzingatia hali halisi ya utoaji wa elimu hiyo kwa sasa, hususan upungufu mkubwa sana wa walimu wenye sifa stahiki waliopo shuleni na kwenye soko la ajira, Kamati inapendekeza elimu hii isiwe ya lazima kwa sasa. Kamati inatambua umuhimu wa Elimu ya Awali kwa maendeleo thabiti ya ukuaji na ujifunzaji wa mtoto. Hivyo basi, Kamati inapendekeza kwamba serikali iendelee kuweka mikakati mahususi ikiwemo kuandaa walimu mahiri wa Elimu ya Awali na miundo mbinu rafiki, fikivu na ya kutosha kabla ya kuamua elimu hiyo kuwa ya lazima.

### 5.2.2 Elimu ya Msingi

Elimu ya Msingi itatolewa kwa muda wa miaka sita (6) na itakuwa na hatua mbili. Hatua ya kwanza itatolewa kwa muda wa miaka miwili na itajumuisha Darasa la Kwanza na Darasa la Pili. Lengo kuu la hatua hii ni kujenga umahiri katika stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Hatua ya pili itaanzia Darasa la Tatu hadi la Sita na italenga kuimarisha stadi za KKK pamoja na stadi nyingine za maisha kupitia masomo ya Jiografia na Mazingira, Kiswahili, Sanaa na Michezo, Hisabati, Sayansi, Historia ya Tanzania na Maadili, Dini na Kiingereza. Pia, mwanafunzi atajifunza Stadi za Kazi ambazo maudhui yake yatachopekwa katika Somo la Sanaa na Michezo na katika masomo mengine. Ili kuimarisha umahiri wa lugha, Kamati inashauri kuhamasisha shule zenye uwezo kufundisha walau somo moja chaguzi la lugha ya kigeni (mfano Kifaransa, Kichina na Kiarabu). Aidha, Kamati inapendekeza Kiingereza kifundishwe kuanzia Darasa la Kwanza kwa shule zinazotumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia na Kiswahili kifundishwe kuanzia Darasa la Kwanza kwa shule zinazotumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia.

RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 15 08/05/2023 15:04

Kama ilivyoelezwa awali, Kamati inapendekeza kusiwe na mtihani wa kumaliza Darasa la Sita (*Primary School Leaving Examination, PSLE*), badala yake kuwe na upimaji wa kitaifa wa Darasa la Sita. Lengo ni kumwezesha kila mwanafunzi aliyefikia kiwango fulani cha umahiri kuendelea na Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini.

### 5.2.3 Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini


Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini itatolewa kwa muda wa miaka minne na itagawanyika katika mikondo miwili: Mkondo wa Elimu ya Jumla na Mkondo wa Elimu ya Amali. Kila shule ya sekondari ya chini italazimika kuwa na mkondo wa Elimu ya Jumla na mkondo wa Elimu ya Amali. Mwanafunzi atachagua mkondo kulingana na matakwa, uwezo na malengo yake ya maisha. Faida ya kila shule kuwa na mikondo yote ni kutoa fursa pana kwa kila mwanafunzi kuchagua kufuata mkondo anaoutaka. Mwanafunzi atakayepitia mkondo wa Elimu ya Amali atakuwa na uwezo wa kuajiriwa au kujiajiri mara baada ya kuhitimu Kidato cha Nne. Aidha, atakuwa na fursa ya kujiendeleza kielimu kupitia vyuo vya elimu ya Ufundi Sanifu kama ilivyofafanuliwa katika Kielelezo Na. 2.

Mkondo wa Elimu ya Amali utagawanyika katika michepuo ya fani mbalimbali kama Kilimo na ufugaji, Umakenika, Biashara na ujasiriamali, Sanaa Bunifu, Elimu ya Michezo, Ufugaji wa nyuki, Uchimbaji madini, Urembo, n.k kama ilivyoainishwa kwenye Kielelezo Na. 3 na Kiambatisho Na. 4. Wanafunzi katika mkondo huu pia watatakiwa kusoma masomo mengine ya jumla ili kupata stadi za msingi katika mawasiliano, stadi za maisha na uzalendo. Masomo yanayopendekezwa ni Hisabati, Elimu ya Biashara, Kiingereza, na Historia ya Tanzania na Maadili. Somo la Elimu ya Biashara (*Business Studies*) limependekezwa kuwa la lazima ili limfundishe mwanafunzi mbinu na mikakati ya kutumia ujuzi alioupata katika fani yake ya Elimu ya Amali kuanzisha na kuendesha biashara kwa ufanisi. Kwa mantinki hiyo, somo hilo limesukwa upya kwa kuingiza maudhui yanayohusu misingi ya ujasiriamali, mbinu za kutambua fursa za kibiashara, namna ya kuanzisha na kuendesha biashara ndogo ndogo, sera na sheria zinazohusu biashara ndogo, vyanzo vya mitaji na kadhalika. Kuanzishwa kwa somo hili kumepelekea kufutwa kwa somo la *Commerce* kwani malengo ya masomo hayo yanafanana.

RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 16 08/05/2023 15:04




**Kielelezo Na. 3:** *Michepuo ya Fani Mbalimbali za Mkondo wa Elimu ya Amali*



Taarifa ya Kamati Final.indd 17 08/05/2023 15:04

Kamati inapendekeza kuwa wahitimu wa mkondo wa Elimu ya Amali wafanye mitihani ya aina mbili na kupewa vyeti viwili: cheti cha kuhitimu elimu ya sekondari na cheti cha Elimu ya Amali kitakachotolewa na Mamlaka husika, kwa sasa, Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi Sanifu na Ufundi Stadi (NACTVET). Hivyo basi, muundo unaopendekezwa unaoanisha sehemu ya mtaala wa vyuo vilivyopo chini ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) na mfumo wa elimu ya sekondari ya hatua ya chini. Mapendekezo haya yana maana kwamba kila shule ya Sekondari Hatua ya Chini mkondo wa Elimu ya Amali itakuwa ni wakala wa VETA. Aidha, kila mwanafunzi wa mkondo huu atachukua masomo manne ya jumla na masomo ya fani moja ya elimu ya amali kwa kutumia mitaala ya VETA. NACTVET itatahini wanafunzi kila wanapomaliza hatua moja ya mafunzo ya Elimu ya Amali. Hii itafanya wahitimu wa Mkondo wa Elimu ya Amali wamalize masomo yao wakiwa na umahiri wa angalau ngazi ya pili (NVA II) ya NACTVET katika fani husika.

Kuifanya kila shule ya sekondari ya Mkondo wa Elimu ya Amali kuwa wakala wa VETA kutasababisha ongezeko kubwa sana la wanafunzi wa Mamlaka hiyo. Kwa sababu ya ongezeko hilo, Kamati inapendekeza VETA na NACTVET ziimarishwe ili ziweze kumudu majukumu ya uthibiti ubora wa elimu ya amali iliyopanuka kwa sababu ya kutolewa pia katika shule za sekondari. Baadhi ya maboresho yanayopendekezwa ni pamoja na kuimarisha ofisi za kanda na kuongeza idadi ya wafanyakazi na vitendea kazi ili kuweza kuhimili ongezeko la shughuli za utahini, ubunifu na uboreshaji wa mitaala.

Kutokana na umri wa wanafunzi wa shule za sekondari kuwa mdogo ni dhahiri kwamba hawataweza kumudu baadhi ya fani za masomo ya elimu ya amali kama vile *Heavy Duty Equipment, Scaffolding, Mining* na kadhalika. Kwa sababu hiyo, fani hizo zitaendelea kutolewa na vyuo vya VETA peke yake. Aidha, vyuo vya VETA vitaendelea kutoa kozi zake zote kwa wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu wanaotafuta kupata umahiri katika stadi za elimu ya amali mahsusi kulingana na matakwa yao na fursa za kiuchumi zilizopo ili kutimiza dhana ya elimu bila ukomo. Pia, inapendekezwa kwamba VETA itoe mafunzo yatakayowezesha wahitimu kupata vyeti vya ubobezi katika fani mbalimbali za elimu ya amali (*high-level certification in specific vocations*) kulingana na mahitaji ya soko.

Baada ya kumaliza Kidato cha Nne, wanafunzi wa shule za Sekondari Hatua ya Chini mkondo wa Elimu ya Amali wataweza kujiunga na maisha ya kazi moja kwa moja kwani elimu hiyo itakuwa imewapatia umahiri wa kazi wa kutosha. Wale watakaohitaji kuongeza umahiri wao katika elimu ya amali wataweza kujiunga na vyuo vya elimu ya amali sanifu kwa mafunzo ya stashahada ya miaka

mitatu (3) ambayo watahitimu kama *technicians/para-professionals*. Aidha, wale wenye ufaulu stahiki wataweza kujiunga na elimu ya Amali ya Juu (*technical higher education*) ambapo watahitimu kama wataalamu (*professionals*) katika fani husika kama ilivyofafanuliwa katika Kielelezo Na. 2.

Ili kuongeza tija katika mfumo wetu wa elimu inapendekezwa kwamba mamlaka husika zitoe ufafanuzi bayana wa malengo ya mikondo ya elimu ya juu ya jumla (*general higher education*), ambayo kwa sasa inasimamiwa na Tume ya Vyuo Vikuu (*Tanzania Commission for Universities*, *TCU*), na yale ya mkondo wa elimu ya juu ya amali (*technical higher education*) ambayo kwa sasa inasimamiwa na NACTVET. Ufafanuzi huu ubainishe umahiri unaohitajika katika kila mkondo na hivyo kuongoza uandaaji wa mitaala yenye tija kwa maendeleo ya Taifa. Ufafanuzi huu utaondoa dhana kwamba mikondo hii ni njia mbadala tu ya kupata elimu ya juu badala ya ukweli kwamba ni njia zinazosaidiana (*complementary pathways*) kuandaa mchanganyiko wa umahiri katika nyanja mbalimbali (*skill mix*) unaohitajika katika kuleta maendeleo ya Taifa letu. Aidha, Kamati inapendekeza kwamba mamlaka husika kwa pamoja ziandae vigezo vitakavyohakikisha wahitimu kutoka ngazi moja wanaweza kuendelea na mafunzo katika ngazi nyingine kama ilivyooneshwa katika Kielelezo Na. 2.

Ili kurahisisha utoaji wa elimu ya amali, Kamati inapendekeza kwamba shule yoyote isiwe na michepuo zaidi ya miwili ya elimu ya amali. Pia, aina ya michepuo itakayotolewa katika shule mbalimbali izingatie shughuli za uchumi na fursa zilizopo katika maeneo husika na iwe inapitiwa upya kila baada ya muda ili kuhakikisha inaendana na matakwa ya wakati. Aidha, mwanafunzi wa mkondo wa Elimu ya Amali atakuwa na uhuru wa kuchagua masomo ya ziada ya jumla kulingana na uwezo wake na ratiba ya shule husika.

Mfumo wa elimu uliopo unajumuisha shule za sekondari tisa (9) za umma ambazo ni za mchepuo wa ufundi (Ifunda, Moshi, Tanga, Mtwara, Iyunga, Bwiru, Musoma, Chato na Mwadui) kwa Tanzania Bara. Aidha, kuna shule kama hizo binafsi tatu (3) ambazo ni Ihanja, Minja na Don Bosco. Kwa upande wa Zanzibar, kuna shule mbili (2) za sekondari za ufundi ambazo ni Kengeja Ufundi na Mikunguni. Shule hizo zinafundisha masomo ya jumla kama shule nyingine za sekondari pamoja na masomo ya elimu ya amali katika fani za Uhandisi Mitambo, Umeme, na Ujenzi na hivyo kuwafanya wanafunzi kuchukua masomo yasiyo pungua kumi na nne (14). Mchanganyiko huu wa masomo unawapa mzigo mkubwa sana wanafunzi na hivyo kuwapunguzia ufanisi katika ujifunzaji. Aidha, wanafunzi hawana fursa ya kubobea katika stadi yoyote ya ufundi kiasi cha kufuzu kutunukiwa cheti cha umahiri cha VETA. Wale wanaotaka kufanya mitihani ya VETA inawabidi



Taarifa ya Kamati Final.indd 19 08/05/2023 15:04

wachukue mafunzo ya ziada (*extra tuition*) au kujiunga na vyuo vya VETA baada ya kuhitimu elimu ya sekondari. Njia zote hizi huwaongezea gharama wanafunzi. Changamoto hizo zimesababisha wanafunzi wa sekondari za ufundi kukosa hamasa ya masomo ya ufundi na kujikita zaidi kwenye masomo ya taaluma kwani hayo ndiyo yanawawezesha kujiunga na elimu ya Kidato cha Tano au masomo ya stashahada katika vyuo vya Ufundi Sanifu.


Ili kukabiliana na changamoto zilizopo katika shule za sekondari za ufundi, Kamati inapendekeza kwamba shule hizo ziimarishwe na kugeuzwa kuwa vitovu vya kufundishia elimu ya sekondari ya hatua ya chini mkondo wa Elimu ya Amali katika stadi za kihandisi. Baadhi ya maboresho yanayopendekezwa ni pamoja na kukarabati/kupanua karakana na kuongeza idadi ya walimu wa Elimu ya Amali. Ili kutumia vizuri miundombinu iliyopo, shule hizo zitoe mafunzo ya Elimu ya Amali katika fani zote za uhandisi kwa kutumia mitaala ya VETA kama inavyopendekezwa kwa shule nyingine za Sekondari Hatua ya Chini mkondo wa Elimu ya Amali. Hii ina maana kwamba tofauti na shule nyingine za mkondo wa Elimu ya Amali, shule hizi zitaruhusiwa kutoa zaidi ya fani mbili za Elimu ya Amali. Aidha, idadi ya masomo ya jumla ipunguzwe kuwa manne kama ilivyo kwa shule nyingine za Sekondari Hatua ya Chini mkondo wa Elimu ya Amali. Pia, inapendekezwa kwamba shule hizo ziruhusiwe kuendelea na Mkondo wa Elimu ya Jumla kama ilivyo sasa.

Mkondo wa Elimu ya Jumla utajikita kwenye masomo ya kitaaluma. Katika muundo wa elimu uliopo sasa, wanafunzi wamegawanyika katika michepuo minne ambayo ni Sayansi ya Jamii, Kilimo, Biashara na Sayansi. Kama hatua ya kuongeza unyumbufu katika Mkondo wa Elimu ya Jumla, Kamati inapendekeza kuongeza idadi ya michepuo kutoka minne ya sasa hadi tisa (09). Michepuo mipya inayopendekezwa ni Sanaa, Lugha, Muziki, Michezo na TEHAMA kama ilivyofafanuliwa katika Kielelezo Na. 4. Michepuo mipya iliyopendekezwa inalenga kuwajengea wahitimu wa Mkondo wa Elimu ya Jumla uwezo wa kushiriki moja kwa moja katika ulimwengu wa kazi kupitia masomo chaguzi watakayochukua.

Aidha, mwanafunzi ataweza kujifunza masomo yote ya jumla akiwa Kidato cha Kwanza na cha Pili. Kuanzia Kidato cha Tatu mwanafunzi atachagua masomo katika moja ya michepuo kulingana na matakwa, uwezo na malengo yake ya maisha. Licha ya masomo katika michepuo yao, wanafunzi wote wa Mkondo wa Elimu ya Jumla wataweza kuchagua masomo ya ziada, yakiwamo yale ya Mkondo wa Elimu ya Amali, kulingana na ratiba na uwezo wa shule husika. Lengo kuu la mkondo huu ni kuandaa vijana kwa ajili ya elimu ya juu ili kulipatia taifa wataalamu mbalimbali wakiwemo madaktari, wahandisi, wanasheria, wachumi, watafiti na kadhalika.



Taarifa ya Kamati Final.indd 20 08/05/2023 15:04




**Kielelezo Na. 4:** *Michepuo Mipya Inayopendekezwa*




Taarifa ya Kamati Final.indd 21 08/05/2023 15:04

### 5.2.4 Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu

Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu itajikita kwenye masomo ya jumla yatakayotolewa katika tahasusi ili kumuandaa mhitimu kujiunga na elimu ya juu. Elimu hiyo itatolewa kwa muda wa miaka miwili. Idadi na aina ya tahasusi zitakuwa zinapitiwa mara kwa mara kuhakikisha zinakidhi mahitaji halisi ya Taifa katika wakati husika. Ili kuongeza wigo wa fursa za kujiunga na elimu ya juu, inapendekezwa kwamba idadi ya masomo katika kila tahasusi isiwe chini ya matatu na wala isizidi manne kulingana na uwezo na malengo ya mwanafunzi. Aidha, aina ya masomo katika kila tahasusi izingatie malengo ya kitaalamu (*career aspirations and pathways*) ya wahitimu na rasilimali zilizopo shuleni. Pia, kama ilivyo kwa wanafunzi wa Sekondari Hatua ya Chini, wanafunzi wote wa mkondo wa Elimu ya Jumla wawe huru kuchagua masomo ya ziada, yakiwemo yale ya Mkondo wa Elimu ya Amali, kulingana na ratiba na uwezo wa shule husika ili kuwaongezea umahiri utakaowawezesha kumudu maisha yao baada ya kuhitimu.

## 5.3 Uthibiti Ubora

*Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014* kama ilivyorekebishwa Mwaka 2023, inasisitiza umuhimu wa kuimarisha mifumo ya usimamizi wa uthibiti ubora wa elimu katika ngazi zote. Ili kutekeleza lengo hilo na kuhakikisha kwamba mapendekezo yote kuhusu muundo wa elimu na mitaala yanatekelezwa ipasavyo, Kamati inapendekeza kiundwe chombo thabiti cha kusimamia ubora wa elimu ya msingi, sekondari na elimu ya ualimu kama ilivyo kwa elimu ya juu na elimu ya ufundi nchini.

RASIMU

# 6.0 Mapendekezo Kuhusu Mitaala

Kwa kuzingatia maoni ya wadau, sera, falsafa na matamko mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, Kamati inapendekeza maboresho ya misingi itakayoongoza mapitio ya mitaala kama ifuatavyo:

## 6.1 Dira na Malengo Makuu ya Elimu

Katika sehemu zinazofuata, Kamati inatoa muhtasari wa dira, malengo makuu na malengo ya kila ngazi pendekezwa ya elimu.

### 6.1.1 Dira ya Elimu

Dira ya Elimu yetu ni kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo katika kuleta maendeleo endelevu ya kitaifa na kimataifa.

### 6.1.2 Malengo Makuu ya Elimu

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(i) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini.

(ii) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi.

(iii) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla.

(iv) Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa.

(v) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku.

(vi) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma.

(vii) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira.

RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 23 08/05/2023 15:04

(viii) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 6.2 Malengo ya Elimu kwa Kila Ngazi

Kutokana na Dira na Malengo makuu ya elimu kama yalivyobainishwa katika sehemu ya 6.1, yafuatayo ni malengo ya elimu kwa kila ngazi ya elimu:

### 6.2.1 Malengo ya Elimu ya Awali

Malengo ya Elimu ya Awali ni:

(i) Kujenga misingi imara ya makuzi ya kimwili na uratibu wa misuli mikubwa na midogo.

(ii) Kukuza maadili na uwezo wa mtoto kuthamini na kudumisha tunu za taifa na utamaduni wa jamii yake.

(iii) Kukuza stadi za awali za lugha na mawasiliano (kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika), Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), lugha mguso, na maandishi ya Breli.

(iv) Kukuza stadi za awali za ujifunzaji wa mtoto na tabia ya kupenda kujifunza.

(v) Kujenga uwezo wa mtoto kijamii na kihisia.

(vi) Kukuza urazini na ujumi wa mtoto katika kutunza afya na mazingira.

(vii) Kukuza stadi za awali za kihisabati, kufikiri kimantiki, kutatua matatizo, ubunifu, uvumbuzi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

(viii) Kubaini mtoto mwenye mahitaji maalumu na kutoa afua stahiki.

(ix) Kumwezesha mtoto kuvuka salama kipindi cha mpito kutoka darasa la awali kwenda darasa la kwanza.

### 6.2.2 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la Kwanza hadi la Pili

Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la Kwanza hadi la Pili ni kumwezesha mwanafunzi:

(i) Kukuza stadi za Kusoma, Kuandika, na Kuhesabu (KKK), ikihusisha kutumia maandishi ya Breli, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso.

(ii) Kukuza uwezo wa kuwasiliana kwa njia stahiki ikiwemo Teknolojia ya



RASIMU

Taarifa ya Kamati Final.indd 24 08/05/2023 15:04

Habari na Mawasiliano na teknolojia saidizi.

(iii) Kujenga uimara wa mwili, kukuza vipaji, kushirikiana na wenzake na kuwa na mtazamo chanya kuhusu kujifunza.

(iv) Kukuza urazini na ujumi, kupenda na kutunza afya na mazingira pamoja na rasilimali zilizopo.

(v) Kukuza maadili na uwezo wa kuthamini na kudumisha tunu za Taifa na utamaduni wa jamii yake pamoja na kutambua tofauti za tamaduni mbalimbali.

(vi) Kukuza uwezo wa kuchangamana katika mazingira jumuishi.

### 6.2.3 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la Tatu hadi la Sita

Malengo ya Elimu Msingi Darasa la Tatu hadi la Sita ni kumwezesha mwanafunzi:

(i) Kukuza stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso.

(ii) Kufahamu, kutumia na kuthamini lugha za Kiswahili na Kiingereza. Aidha, mwanafunzi ahamasishwe kumudu angalau lugha nyingine moja ya kigeni kulingana na hali halisi ya shule yake.

(iii) Kuthamini na kudumisha utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine.

(iv) Kukuza maarifa, uwezo wa kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo.

(v) Kukuza maadili, uadilifu, na kuheshimu tofauti za imani.

(vi) Kubaini na kukuza vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa.

(vii) Kukuza tabia ya kuthamini na kupenda kufanya kazi.

(viii) Kutambua na kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na katika maisha ya kila siku.

(ix) Kukuza maarifa, ujuzi na mwelekeo wa kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka.

(x) Kukuza uwezo wa kuchangamana katika mazingira jumuishi.

### 6.2.4 Malengo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini – Elimu ya Jumla

Malengo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini (Elimu ya Jumla) ni:

(i) Kuimarisha, kupanua na kuendeleza uelewa wa kina wa maarifa, stadi



Taarifa ya Kamati Final.indd 25 08/05/2023 15:04

na mwelekeo alioupata katika ngazi ya Elimu ya Msingi.

(ii) Kulinda mila na desturi, umoja wa kitaifa, tunu za Taifa, demokrasia, kuthamini haki za binadamu na za kiraia, wajibu na majukumu yanayoendana na haki hizo.

(iii) Kukuza tabia ya kujiamini na uwezo wa kujifunza kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia, na kiufundi.

(iv) Kuimarisha mawasiliano kwa kutumia stadi za lugha ikiwemo Lugha ya Alama Tanzania (LAT), lugha mguso, lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Aidha, mwanafunzi ahamasishwe kumudu angalau lugha nyingine moja ya kigeni kulingana na hali halisi ya shule yake.

(v) Kuimarisha uwajibikaji katika masuala mtambuka ya kijamii yakiwemo afya, usalama, usawa wa kijinsia, na utunzaji endelevu wa mazingira.

(vi) Kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake.

(vii) Kukuza utayari wa kujiendeleza na mafunzo ya elimu ya kati na ya juu.

### 6.2.5 Malengo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini – Elimu ya Amali

Malengo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini (Elimu ya Amali) ni:

(i) Kuimarisha, kupanua na kuendeleza uelewa wa kina wa maarifa, stadi, na mwelekeo alioupata katika ngazi ya elimu ya msingi.

(ii) Kukuza stadi za ufundi na ujasiriamali zitakazomwezesha kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake.

(iii) Kulinda mila na desturi, umoja wa kitaifa, tunu za Taifa, demokrasia, kuthamini haki za binadamu na za kiraia, wajibu na majukumu yanayoendana na haki hizo.

(iv) Kuimarisha mawasiliano kwa kutumia stadi za lugha.

(v) Kukuza tabia ya kujiamini na uwezo wa kujifunza kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia, na kiufundi.

(vi) Kuimarisha uwajibikaji katika masuala mtambuka ya kijamii yakiwemo afya, usalama, usawa wa kijinsia, na utunzaji endelevu wa mazingira.



Taarifa ya Kamati Final.indd 26 08/05/2023 15:04

RASIMU

(vii) Kukuza utayari wa kujiendeleza na Mafunzo ya Elimu ya Amali na Sanifu.

### 6.2.6 Malengo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu

Malengo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu ni:

(i) Kuimarisha, kupanua na kuendeleza uelewa wa kina wa maarifa, stadi, na mwelekeo alioupata katika ngazi ya elimu ya Sekondari Hatua ya Chini.

(ii) Kulinda mila na desturi, tunu za Taifa, demokrasia, kuthamini haki za binadamu na za kiraia, na wajibu na majukumu yanayoendana na haki hizo.

(iii) Kukuza tabia ya kujiamini na uwezo wa kujifunza kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia, na kiufundi.

(iv) Kuimarisha matumizi ya lugha katika mawasiliano ya kitaaluma.

(v) Kuimarisha uwajibikaji katika masuala mtambuka ya kijamii yakiwemo afya, usalama, usawa wa kijinsia, na utunzaji endelevu wa mazingira.

(vi) Kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake.

(vii) Kumwandaa mwanafunzi kujiunga na vyuo vya elimu ya kati.

RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 27 08/05/2023 15:04

# 7.0 Umahiri wa Jumla na Masomo kwa kila Hatua ya Elimu

## 7.1 Utangulizi

Kutokana na Dira na malengo ya elimu katika ngazi mbalimbali, maboresho ya mitaala yanayopendekezwa yamejikita katika ujenzi wa umahiri wa msingi katika kuwasiliana, kushirikiana, ubunifu, fikra tunduizi na utatuzi wa matatizo, ujuzi wa kidijitali, maadili na uzalendo (Stadi za Karne ya 21) kwa kuzingatia falsafa ya Elimu ya Kujitegemea. Katika kutafsiri malengo haya katika umahiri wa jumla, maeneo ya ujifunzaji, masomo, umahiri mahsusi na mihtasari kwa kuzingatia maoni ya wadau, mifano bora kutoka mataifa mbalimbali na hali halisi ya nchi yetu, Kamati iliongozwa na misingi kama ifuatavyo:

### 7.1.1 Kuwasiliana

Kukuza uwezo wa kuwasiliana kumeainishwa kama moja ya malengo makuu ya elimu Tanzania. Hata hivyo, wadau mbalimbali wameonesha kutoridhishwa na uwezo wa wahitimu katika kuwasiliana kwa Kiswahili na Kiingereza. Aidha, ni ukweli usiopingika kwamba Watanzania wengi hawana uelewa wa lugha nyingine za kigeni zaidi ya Kiingereza licha ya umuhimu wa lugha hizo katika biashara na mahusiano mengine ya kikanda na ya kimataifa. Kamati imebaini kwamba tatizo hilo limechangiwa kwa kiasi kikubwa na namna masomo ya lugha yanavyofundishwa. Kwa sababu hiyo, Kamati inapendekeza kubadilisha namna masomo ya lugha yanavyofundishwa kwa kusisitiza ujenzi wa umahiri wa lugha yenyewe kabla mwanafunzi hajaanza kuitumia katika mawasiliano tofauti na mfumo uliopo sasa. Aidha, Kamati inapendekeza lugha ya Kiingereza ianze kufundishwa kuanzia Darasa la Kwanza kwa shule zinazotumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia. Vilevile, inapendekezwa kwamba lugha ya Kiswahili ianze kufundishwa kuanzia Darasa la Kwanza kwa shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia.

Mapendekezo mengine yanayolenga kuboresha umahiri wa kuwasiliana ni pamoja na kuanzisha masomo chaguzi ya lugha za kigeni kuanzia ngazi ya Elimu ya Msingi, kuanzisha mchepuo wa masomo ya lugha katika Elimu ya Sekondari na kuanzisha somo jipya la lazima la Mawasiliano ya Kitaaluma katika Elimu ya



Taarifa ya Kamati Final.indd 28 08/05/2023 15:04

Sekondari Hatua ya Juu na Elimu ya Ualimu. Aidha, umahiri wa kuhariri, kutafsiri na kukalimani umeingizwa katika masomo yote ya lugha. Vilevile, umahiri wa kuwasiliana kitaaluma na kutafuta maarifa kwa kutumia TEHAMA umeingizwa kwenye somo la Kiingereza ambalo ni la lazima katika ngazi zote za elimu.

### 7.1.2 Ubunifu, Fikra Tunduizi na Utatuzi wa Matatizo

Ubunifu, fikra tunduizi, tafakuri na uwezo wa kutatua matatizo ni umahiri unaohitajika sana ili kuleta maendeleo katika ulimwengu wa sasa. Ili kujenga umahiri huu kwa wanafunzi wetu, Kamati inapendekeza kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia mbinu zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji. Mbinu zinazopendekezwa ni shirikishi zikiwemo zile zinazomwezesha mwanafunzi kufikiri, kutafakari, kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali, kazi za vitendo, utafiti, majaribio ya kisayansi, majadiliano na kazimradi zinazolenga kutatua matatizo halisi katika mazingira ya mwanafunzi. Aidha, Kamati inapendekeza kuimarisha upimaji endelevu na tamati kwa kutumia zana na mbinu zinazopima nadharia na vitendo. Mfumo wa upimaji utumie vigezo vinavyotambulika vya upimaji wa maendeleo ya kila siku ya mwanafunzi na tathmini ya mwisho ya kukamilisha ngazi husika kwa kuzingatia mtaala wa ujenzi wa umahiri. Mbinu na njia hizi zimezingatiwa katika uandaaji wa mitaala iliyopendekezwa.

Kamati inatambua umuhimu wa Hisabati katika kujenga uwezo wa kufikiri kimkakati, kutatua matatizo na kumudu sayansi na teknolojia. Kwa sababu hiyo mitaala italenga katika kukuza umahiri katika hisabati katika ngazi zote za elimu. Aidha, mitaala inasisitiza kujenga umahiri wa kinadharia na kimatendo katika masomo yote ya sayansi na teknolojia kwa lengo la kukuza ubunifu.

### 7.1.3 Ujuzi wa Kidijitali

Ujuzi wa kidijitali ni mojawapo ya stadi muhimu za Karne ya 21 ambazo zimeainishwa bayana katika malengo ya elimu ya Tanzania. Ili kufanya mitaala yetu ikidhi mahitaji ya sasa, Kamati inapendekeza matumizi ya TEHAMA katika kutatua matatizo ya kitaaluma yafundishwe kwa kuyachopeka wakati wa vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji katika masomo yote kuanzia ngazi ya Elimu ya Awali. Vilevile, Kamati inapendekeza maudhui yanayohusu utengenezaji wa programu za kompyuta (*coding*) yaingizwe katika mtaala wa Somo la Sayansi katika Elimu ya Msingi. Aidha, somo la *Information and Computer Studies* limesukwa upya kwa kujikita zaidi katika kufundisha sayansi. Kwa sababu

RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 29 08/05/2023 15:04

hiyo, somo hilo limebadilishwa jina na kuwa *Computer Science*. Somo hilo pia limeundiwa mchepuo mpya wa TEHAMA katika ngazi ya Sekondari Hatua ya Chini.

### 7.1.4 Kushirikiana na Uzalendo

Ili kufanikiwa katika ulimwengu wa sasa ni muhimu wahitimu wawe na uwezo wa kushirikiana katika miktadha mbalimbali. Aidha, ni dhahiri kwamba uzalendo na uadilifu ni sifa muhimu za kuwa raia mwema mwenye kuwajibika kwa jamii yake. Kwa sababu hiyo, Kamati inapendekeza kuchopeka umahiri wa kushirikiana kupitia vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji katika masomo ya ngazi zote za elimu. Pia, Kamati inapendekeza kuunganisha masomo ya Uraia, *Civics* na Historia ya Tanzania kuwa somo moja linaloitwa Historia ya Tanzania na Maadili. Somo hili limebeba maudhui yanayolenga kumjenga Mtanzania mzalendo na muwajibikaji anayefahamu historia, desturi, mila na maadili ya nchi yake. Aidha, inapendekezwa kwamba mada zinazosisitiza uzalendo, uwajibikaji na maadili zichopekwe kwenye masomo bebezi katika ngazi mbalimbali za elimu.

Katika kuhakikisha kwamba tunajenga jamii inayothamini usawa na haki, Kamati inapendekeza kwamba masuala yanayohusu mitazamo na matendo jumuishi yachopekwe katika mitaala ya masomo yote kuanzia ngazi ya Elimu ya Awali.

Aidha, katika kuongeza msisitizo kwenye maadili na uzalendo, Kamati imeendelea kuzingatia elimu ya imani ya dini miongoni mwa umahiri wa jumla, maeneo ya ujifunzaji na masomo katika ngazi zote za elimu. Vilevile, masomo ya dini katika ngazi ya sekondari yamesukwa upya kwa kushirikiana na viongozi wa dini husika kuhakikisha kuwa yanasaidia kujenga tunu muhimu za Taifa ikiwemo uzalendo, uadilifu, maadili mema na uchapakazi.

### 7.1.5 Wingi wa Maudhui

Wadau walionesha dukuduku la wingi wa maudhui katika mitaala iliyopo. Ni dhahiri kwamba wingi wa maudhui katika mitaala unaathiri ufundishaji na ujifunzaji kulingana na muda uliopangwa katika ratiba. Tatizo hilo linasababisha utekelezaji wa mitaala kutokamilika kwa muda uliopangwa na wanafunzi kukosa muda wa kutafakari na kujenga stadi nyingine za maisha nje ya darasa. Kamati imebaini kwamba, kumekuwa na mtindo wa kuongeza maudhui mapya katika



Taarifa ya Kamati Final.indd 30 08/05/2023 15:04

mitaala kila jambo jipya linapojitokeza katika jamii bila kuzingatia kwamba muda wa kufundisha na kujifunza haujaongezeka. Hata hivyo, kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa mitaala inaendelea kukidhi mahitaji ya wanafunzi na jamii. Aidha, ni muhimu kuhakikisha kwamba mitaala inaendana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia kwa kuzingatia mazingira na mahitaji halisi ya nchi. Ili kukabiliana na tatizo la utanuzi holela wa mitaala, Kamati inapendekeza kupunguza wingi wa maudhui na kuongeza ubora wa mitaala kama ifuatavyo:

(i) Kuboresha mitaala yote kwa kuongeza maudhui ya kisasa, kuondoa maudhui yaliyopitwa na wakati na kuondoa kujirudiarudia kwa maudhui katika somo na baina ya masomo.

(ii) Kupunguza wingi wa maudhui katika kila somo ili uwiane na muda wa kufundishia na mahitaji ya halisi ya jamii yetu kwa kuzingatia mifano bora (*best practices*) kutoka mataifa mbalimbali.

(iii) Kupunguza idadi ya masomo ya lazima katika ngazi ya Sekondari Hatua ya Chini kutoka saba (7) hadi sita (6) kwa kuyafanya masomo ya *Biology* na *Geography* kuwa chaguzi kwa sababu maudhui yake muhimu yamejumuishwa kwenye masomo ya Sayansi na Jiografia na Mazingira mtawalia katika Elimu ya Msingi. Maudhui hayo, ambayo ndiyo yalisababisha *Biology* kuwa somo la lazima, yanahusu afya ya jamii, chakula na lishe, afya ya uzazi, na magonjwa ya kuambukiza na ya mlipuko. Aidha, maudhui muhimu yanayohusu mazingira katika somo la *Geography* yamejumuishwa katika somo la Jiografia na Mazingira. Hatua hii pia itawawezesha wanafunzi kuchukua masomo mengi zaidi chaguzi kutegemeana na uwezo na malengo yao.

(iv) Mwanafunzi aliyefaulu somo la *Additional Mathematics* akiwa Sekondari Hatua ya Chini asilazimike kusoma somo la *Basic Applied Mathematics* katika Sekondari Hatua ya Juu kwa sababu maudhui ya masomo hayo yanafanana. Hatua hii pia itawawezesha wanafunzi kuchukua mojawapo ya somo la ziada la tahasusi kutegemeana na uwezo na malengo yao.

(v) Kuunganisha maudhui ya masomo ya Maarifa ya Jamii na Uraia na Maadili kuwa somo moja la Historia ya Tanzania na Maadili katika ngazi ya Elimu ya Msingi ili kuondoa kujirudia kwa maudhui. Aidha, maudhui ya historia ya Tanzania katika somo la Historia yameunganishwa na yale ya *Civics* kuwa somo la Historia ya Tanzania na Maadili katika ngazi ya Elimu ya Sekondari. Kutokana na mabadiliko haya, masomo ya Maarifa ya Jamii, Uraia na Maadili na *Civics* yamefutwa.

(vi) Kufuta somo la *General Studies* katika ngazi ya Sekondari Hatua ya



Taarifa ya Kamati Final.indd 31 08/05/2023 15:04

Juu na kujumuisha maudhui yake kwenye masomo ya Mawasiliano ya Kitaaluma na Historia ya Tanzania na Maadili ili kupunguza idadi ya masomo na kujirudia rudia kwa maudhui

### 7.1.6 Kuhakikisha Mtaala Unakidhi Mahitaji

Katika kuhakikisha kwamba mtaala unaendelea kukidhi mahitaji, maudhui ya baadhi ya masomo yamebadilishwa na masomo mengine mapya yamependekezwa kama ifuatavyo:

(i) Kufanya idadi ya masomo ya tahasusi katika ngazi ya Sekondari Hatua ya Juu isiwe chini ya matatu na wala isizidi manne kulingana na uwezo na malengo ya mwanafunzi ili kuongeza wigo wa fursa za kujiunga na elimu ya juu kwa wahitimu. Aidha, aina ya masomo katika kila tahasusi izingatie malengo ya kitaalamu (*career aspirations and pathways*) ya wahitimu na rasilimali zilizopo shuleni.

(ii) Kuanzisha masomo mapya chaguzi (*optional subjects*) katika elimu ya Sekondari Hatua ya Chini mkondo wa Elimu ya Jumla yanayotoa fursa kwa mwanafunzi kupata ujuzi utakaomwezesha kujiari au kuajiriwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 4.

(iii) Kuongeza idadi ya michepuo kutoka minne ya sasa hadi tisa (09) katika Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini. Michepuo mipya inayopendekezwa ni Sanaa, Lugha, Muziki, Michezo na TEHAMA na imelenga kuwajengea wahitimu ambao hawataendelea na elimu baada ya ngazi hii uwezo wa kushiriki moja kwa moja katika ulimwengu wa kazi.

(iv) Kusuka upya somo la Biashara (*Commerce*) ili limfundishe mwanafunzi mbinu na mikakati ya kuanzisha na kuendesha biashara kwa ufanisi. Kwa sababu hiyo jina la somo hilo limebadilishwa kuwa Elimu ya Biashara (*Business Studies*) na litakuwa la lazima kwa wanafunzi wote wa ngazi ya Sekondari Hatua ya Chini.

## 7.2 Umahiri wa Jumla, Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo

Umahiri wa jumla, maeneo ya ujifunzaji, masomo na umahiri mkuu kama ilivyotafsiriwa kwa kuzingatia misingi iliyofafanuliwa katika Sehemu 7.1 vimeelezwa katika sehemu zifuatazo za Ripoti hii. Aidha, rasimu za mitaala na mihtasari ya masomo kwa ngazi zote za elimu zimeoneshwa katika viambatisho Na.7 na 8.



Taarifa ya Kamati Final.indd 32 08/05/2023 15:04

### 7.2.1 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Awali

Umahiri wa jumla utakaojengwa na mtoto katika Elimu ya Awali ni:

(i) Kumudu stadi za kisanii, ubunifu na michezo.
(ii) Kuthamini utamaduni wa jamii yake, imani na tunu za Taifa.
(iii) Kumudu stadi za awali za lugha na mawasiliano.
(iv) Kuhusiana.
(v) Kutunza afya na mazingira.
(vi) Kutumia stadi za awali za kihisabati, kisayansi na TEHAMA.

#### 7.2.1.1 Maeneo ya Ujifunzaji

Ili kumwandaa mtoto kwa ajili ya ujifunzaji katika Elimu ya Awali, ni muhimu kumwezesha mtoto kujenga umahiri katika nyanja zote za ukuaji. Maeneo ya ujifunzaji ni kama ifuatavyo:

(i) Utamaduni, Elimu ya Imani, Sanaa na Michezo.
(ii) Lugha na Mawasiliano.
(iii) Stadi za awali za maisha.
(iv) Afya na Mazingira.
(v) Stadi za awali za Kihisabati, Kisayansi na TEHAMA.

Maeneo ya ujifunzaji na umahiri mkuu kwa Elimu ya Awali umebainishwa katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2:** Maeneo ya Ujifunzaji na Umahiri Mkuu Elimu ya Awali

| Na. | Maeneo ya Ujifunzaji | Umahiri Mkuu |
|---|---|---|
| 1. | Utamaduni, Elimu ya Imani, Sanaa na Michezo | Kumudu stadi za kisanii, Ubunifu na Michezo |
| | | Kuthamini utamaduni wa jamii yake, imani na Tunu za Taifa. |
| 2. | Lugha na Mawasiliano | Kumudu stadi za awali za lugha ya mawasiliano |
| 3. | Stadi za Awali za Maisha | Kuhusiana |
| 4. | Afya na mazingira | Kutunza afya na mazingira |
| 5. | Stadi za Awali za Kihisabati, Kisayansi na TEHAMA | Kutumia stadi za awali za kihisabati, kisayansi na TEHAMA |

Vilevile, watoto watajifunza masuala mtambuka kama vile mazingira, afya, jinsia, amani, maadili, haki na wajibu ambayo yatachopekwa kwenye maeneo mbalimbali ya ujifunzaji.

RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 33 08/05/2023 15:04

Maelezo zaidi kuhusu umahiri mkuu kwa kila eneo la ujifunzaji yanapatikana katika Kiambatisho Na. 1.

### 7.2.2 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la Kwanza hadi la Pili

(i) Kutumia stadi za Kusoma, Kuandika, na Kuhesabu (KKK), ikihusisha kutumia maandishi ya Breli, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso.

(ii) Kuwasiliana kwa njia stahiki ikiwemo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na teknolojia zingine saidizi.

(iii) Kushiriki katika vitendo vya kuimarisha mwili, kukuza vipaji, kushirikiana na wenzake na kuwa na mtazamo chanya kuhusu kujifunza.

(iv) Kuonesha urazini na ujumi, kupenda na kutunza afya na mazingira pamoja na rasilimali zilizopo.

(v) Kuonesha maadili, kuthamini na kudumisha tunu za Taifa na utamaduni wa jamii yake pamoja na kutambua tofauti za tamaduni mbalimbali.

(vi) Kuchangamana katika mazingira jumuishi.

#### 7.2.2.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Umahiri Mkuu

Katika hatua ya Elimu ya Msingi Darasa la Kwanza hadi la Pili watoto hawatakuwa na masomo isipokuwa watoto watajenga umahiri mbalimbali kupitia maeneo ya ujifunzaji kama yalivyobainishwa katika Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3:** Maeneo ya Ujifunzaji na Umahiri Mkuu Elimu ya Msingi Darasa la Kwanza hadi la Pili

| Na. | Maeneo ya Ujifunzaji | Umahiri Mkuu |
|---|---|---|
| 1. | Lugha, mawasiliano na stadi za hisabati | Kusoma |
| | | Kuandika |
| | | Kuhesabu |
| 2. | Utamaduni, imani, sanaa na michezo | Kuthamini Utamaduni, Imani, Sanaa na Michezo |
| 3. | Afya na mazingira | Kutunza Afya na Mazingira |

Maelezo zaidi kuhusu umahiri mkuu kwa kila eneo la ujifunzaji yanapatikana katika Kiambatisho Na. 2.

### 7.2.3 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la Tatu hadi la Sita

(i) Kutumia stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso.



Taarifa ya Kamati Final.indd 34 08/05/2023 15:04

(ii) Kutumia na kuthamini lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Aidha, mwanafunzi ahamasishwe kumudu angalau lugha nyingine moja ya kigeni kulingana na hali halisi ya shule yake.

(iii) Kuonesha, kuthamini na kuheshimu utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine.

(iv) Kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo.

(v) Kuonesha uadilifu na kuheshimu tofauti za imani.

(vi) Kutumia vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa katika miktadha mbalimbali.

(vii) Kuthamini na kupenda kufanya kazi.

(viii) Kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na katika maisha ya kila siku.

(ix) Kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka.

(x) Kuchangamana katika mazingira jumuishi.

#### 7.2.3.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Elimu ya Msingi Darasa la Tatu hadi la Sita

Katika hatua ya Elimu ya Msingi Darasa la Tatu hadi la Sita wanafunzi watakuwa na maeneo ya kujifunza na masomo kama yalivyobainishwa katika Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na. 4:** Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo Elimu ya Msingi Darasa la Tatu hadi la Sita

| Na. | Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo |
|---|---|---|
| 1. | Lugha na mawasiliano | Kiswahili |
| | | Kiingereza |
| | | Kichina |
| | | Kiarabu |
| | | Kifaransa |
| 2. | Hisabati | Hisabati |
| 3. | Sayansi ya jamii | Historia ya Tanzania na Maadili |
| | | Jiografia na Mazingira |
| | | Elimu ya Dini |



Taarifa ya Kamati Final.indd 35 08/05/2023 15:04

| Na. | Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo |
|---|---|---|
| 4. | Sayansi na teknolojia | Sayansi |
| 5. | Sanaa na michezo | Sanaa na Michezo |

Maelezo zaidi kuhusu umahiri mkuu na umahiri mahususi kwa kila somo yanapatikana katika Kiambatisho Na. 2.

### 7.2.4 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini – Elimu ya Jumla

(i) Kutumia maarifa na stadi alizozipata katika ngazi ya elimu ya msingi kuimarisha na kupanua uelewa wa masomo ya jumla.

(ii) Kuthamini uraia na tunu za Taifa.

(iii) Kuonesha kujiamini katika kujifunza nyanja mbalimbali zikiwemo Sayansi na Teknolojia, maarifa ya kinadharia na ya kivitendo.

(iv) Kutumia stadi za lugha ikiwemo Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), lugha mguso, lugha ya Kiswahili, Kiingereza na angalau lugha moja nyingine ya kigeni kuwasiliana.

(v) Kutumia maarifa ya masuala mtambuka kuyamudu mazingira yanayomzunguka.

(vi) Kutumia ujuzi na stadi kumwezesha kujiajiri, kuajiriwa na kuyamudu maisha na mazingira yanayomzunguka.

#### 7.2.4.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini – Elimu ya Jumla

Katika Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini - Elimu ya Jumla wanafunzi watakuwa na maeneo ya kujifunza na masomo kama yalivyobainishwa katika Jedwali Na. 5.

**Jedwali Na. 5:** Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini- Elimu ya Jumla

| Na. | Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo ya Jumla (*Core and Elective Subjects*) | Masomo chaguzi |
|---|---|---|---|
| 1. | Sayansi Asilia, Teknolojia na Mazingira | Biolojia | Kilimo* |
| | | Fizikia | Sayansi ya Kompyuta* |
| | | Kemia | |



Taarifa ya Kamati Final.indd 36 08/05/2023 15:04

| Na. | Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo ya Jumla (*Core and Elective Subjects*) | Masomo chaguzi |
|---|---|---|---|
| 2. | Sayansi Jamii, Imani na Maadili | Historia | Elimu ya Dini ya Kikristo |
| | | Jiografia | Elimu ya Dini ya Kiislamu |
| | | Historia ya Tanzania na Maadili | |
| 3. | Hisabati | Hisabati | Additional Mathematics |
| 4. | Lugha na Mawasiliano | Kiswahili | Kifaransa |
| | | Kiingereza | Kichina |
| | | | Kiarabu |
| | | | Literature in English |
| | | | Fasihi ya Kiswahili |
| 5. | Elimu ya Amali, Ujasiriamali na Uchumi | Elimu ya Biashara | Elimu ya Amali* |
| | | Utunzaji wa Taarifa za Fedha | Ushoni* |
| | | | Maarifa ya Nyumbani* |
| | | | Chakula na Lishe* |
| | | | Muziki* |
| | | | Michezo* |
| | | | Sanaa Sanifu* |
| | | | Sanaa za Maonyesho* |

** Masomo yanayomtayarisha mwanafunzi kuweza kujiajiri/kuajiriwa mara tu baada ya kuhitimu.*

Maelezo zaidi kuhusu umahiri mkuu na umahiri mahususi kwa kila somo yanapatikana katika Kiambatisho Na. 3.

### 7.2.5 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini – Elimu ya Amali

(i) Kutumia maarifa, stadi na mwelekeo alioupata ngazi ya elimu ya msingi ili kukuza uelewa na stadi za elimu ya amali.

(ii) Kutumia stadi za elimu ya amali katika kubuni, kuvumbua na kutengeneza vitu mbalimbali ili kuyamudu maisha yake na kutatua changamoto katika jamii.

(iii) Kuthamini uraia na tunu za Taifa.

(iv) Kutumia stadi za lugha.



Taarifa ya Kamati Final.indd 37 08/05/2023 15:04

(v) Kuonesha kujiamini katika ujifunzaji katika nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa na stadi za amali.

(vi) Kuthamini taratibu na kanuni za usalama (*safety rules and regulations*) katika kutumia zana za ufundi kwa usahihi.

(vii) Kutumia maarifa na stadi za amali alizozipata ili kujiendeleza na mafunzo ya elimu ya amali na kuingia katika maisha ya kazi.

### 7.2.5.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini – Elimu ya Amali

Katika Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini - Elimu ya Amali wanafunzi watajifunza Fani Mahususi moja kati ya Fani zinazobainishwa katika Jedwali Na. 6.

**Jedwali Na. 6:** Orodha ya Fani Mbalimbali za Elimu ya Amali - Sekondari Hatua ya Chini

| Na. | Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo |
|---|---|---|
| 1. | Electrical Engineering | Electrical installation |
| | | Bio-energy installation |
| | | Wind power plants installation |
| | | Solar enery installation |
| | | Electronic repair** |
| 2. | Mechanical Engineering | Welding and fabrication |
| | | Air conditioning and refrigeration |
| | | Fitter machinist |
| | | Fitter mechanics |
| | | Ginnery fitting |
| 3. | Civil Engineering | Masonry and brick-laying |
| | | Civil drafting |
| | | Boat building |
| | | Carpentry and joinery |
| | | Plumbing and pipe fitting |
| | | Painting and sign writing |
| | | Steel fixing |
| | | Well drilling |
| | | Wood carving** |



Taarifa ya Kamati Final.indd 38 08/05/2023 15:04

| Na. | Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo |
|---|---|---|
| 4. | Automotive Engineering | Motor vehicle mechanics |
| | | Auto-electric |
| | | Auto-body repair |
| | | Motor-cycle and tri-cycle mechanics |
| | | Agro-mechanics |
| 5. | Transport and Logistics | Transport operations |
| | | Clearing and forwarding |
| 6. | Clothing and Textile | Handloom weaving |
| | | Finishing craft |
| | | Basic knitting |
| | | Designing, sewing and cloth technology (DSCT) |
| | | Leather goods and footwear production |
| 7. | Agriculture and Food Processing | Meat processing and technology |
| | | Oil seed processing |
| | | Animal health and production |
| | | Horticulture and field crop production |
| | | Field crop production attendant |
| | | Wood processing |
| | | Bee keeping |
| | | Fishing and fish processing |
| | | Aquaculture and fish processing |
| | | Seaweed farming** |
| 8. | Hospitality and Tourism | Front office operations |
| | | Housekeeping |
| | | Food production |
| | | Food and beverage sales and services |
| | | Tour guide |
| 9. | Commercial and Business Support Services | Business operation assistance |
| | | Secretarial |
| | | Insurance |
| | | Wholesale and retailing |
| | | Geospatial technology |

RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 39 08/05/2023 15:04

| Na. | Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo |
|---|---|---|
| 10. | Printing | Packaging printing |
| | | Screen printing |
| | | Binding and print finishing |
| 11. | Extraction and Processing of Minerals | Jewellery |
| | | Salt extraction |
| | | Gemology (Gemstone cutting, polishing and carving) |
| 12. | Cosmetology | Hair dressing |
| | | Beauty therapy |
| | | Fitness and nutrition |
| 13. | Creative Arts* | Theatre Arts |
| | | Music |
| | | Fine Art |
| | | Film and TV Production |
| 14. | ICT and Electronics** | Computer maintenance |
| | | Mobile phone repair |
| | | Computer programming |
| | | Computer graphics design |
| | | Office machines maintenance |
| 15. | Sports* | Sports |

* *Mihtasari yake itaandaliwa na TET.*

** Mtaala utatolewa na VTA

Maelezo zaidi kuhusu fani kuu na fani mahususi yanapatikana katika Viambatisho Na. 7. na Na. 8.

### 7.2.6 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu

Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu ni:

(i) Kutumia maarifa na stadi alizozipata katika ngazi ya elimu ya Sekondari Hatua ya Chini kuimarisha na kupanua uelewa wake wa elimu ya jumla.

(ii) Kuthamini uraia, tunu za Taifa, na haki za binaadamu na za kiraia.

(iii) Kujiamini katika ujifunzaji wa nyanja mbalimbali zikiwemo Sayansi na Teknolojia, maarifa ya kinadharia na ya kivitendo.

(iv) Kutumia stadi za lugha katika kufanya mawasiliano ya kitaaluma.

(v) Kutumia maarifa ya masuala mtambuka kumudu mazingira yanayomzunguka.



Taarifa ya Kamati Final.indd 40 08/05/2023 15:04

(vi) Kutumia ujuzi na stadi alizozipata kumwezesha kujiajiri, kuajiriwa na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake.

(vii) Kuonesha utayari wa kujiunga na ngazi ya elimu inayofuata.

### 7.2.6.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu

Katika Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu wanafunzi watakuwa na maeneo ya kujifunza na masomo kama yalivyobainishwa katika Jedwali Na. 7.

**Jedwali Na. 7:** Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu

| Na. | Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo |
|---|---|---|
| 1. | Sayansi Jamii | Historia |
| | | Jiografia |
| | | Elimu ya Dini ya Kikristo |
| | | Elimu ya Dini ya Kiislamu |
| | | Historia ya Tanzania na Maadili |
| 2. | Lugha | Kiswahili |
| | | *English* |
| | | *Arabic* |
| | | *French* |
| | | *Chinese* |
| | | Mawasiliano ya Kitaaluma |
| 3. | Sayansi | Fizikia |
| | | Kemia |
| | | Biolojia |
| | | Kilimo |
| | | Chakula na Lishe |
| 4. | Hisabati | Hisabati |
| | | *Basic Applied Mathematics* |
| 5. | Teknolojia | Sayansi ya Kompyuta |
| 6. | Biashara na Uchumi | Uchumi |
| | | Biashara |
| | | Uhasibu |
| 7. | Utamaduni, Sanaa na Michezo | Sanaa Sanifu |

RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 41 08/05/2023 15:04

| Na. | Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo |
|---|---|---|
| | | Muziki |
| | | Sanaa za Maonyesho |
| | | *Textile and Garment Construction* |
| | | Michezo |

Maelezo zaidi kuhusu umahiri mkuu na umahiri mahususi kwa kila somo yanapatikana katika Kiambatisho Na. 4.

RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 42 08/05/2023 15:04

# 8.0 Elimu ya Ualimu

## 8.1 Utangulizi

Mifano mbalimbali duniani imeonesha kwamba ujenzi wa mfumo bora wa elimu unategemea kwa kiasi kikubwa ubora wa walimu wanaouendesha. Aidha, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akisisitiza juu ya umuhimu wa walimu, alisema kwamba "sera yoyote ya elimu, hata iwe nzuri kiasi gani, haiwezi kufanikiwa bila kuwa na walimu walioandaliwa vyema" (Nyerere, 1988). Mwalimu aliendelea kusisitiza kwamba walimu ndiyo waliotwishwa jukumu la kujenga taifa lenye mawazo na mitazamo sahihi kupitia kazi yao ya kurithisha maarifa na maadili kwa vizazi vipya. Kwa mantiki hiyo, ni wazi kwamba ili mabadiliko yoyote ya sera, mfumo na mitaala ya elimu yaweze kuleta tija iliyokusudiwa ni lazima walimu waandaliwe vema. Aidha, ni dhahiri kwamba, ili mitaala itekelezwe kwa ufanisi, ni lazima kuwe na walimu wa kutosha wenye weledi, maadili na ari stahiki. Hii ina maana kwamba, kuna umuhimu wa kuwavutia wahitimu wenye ufaulu wa juu kujiunga na fani ya ualimu kwa kuboresha hadhi, maslahi na mazingira ya kazi kwa walimu.

## 8.2 Mifumo ya Uandaaji wa Walimu

Mfumo wa kuandaa walimu sasa hivi umegawanyika katika ngazi nne: astashahada, stashahada, shahada na stashahada ya uzamili. Walimu wa Elimu ya Awali na Elimu ya Msingi wanatayarishwa katika vyuo vya elimu ya ualimu ambavyo huchukua wahitimu wa Kidato cha Nne na kuwapatia mafunzo ya Astashahada kwa muda wa miaka miwili (2). Mafunzo hayo yanajumuisha maudhui ya masomo ya taaluma (*academic content*) na masomo ya ualimu (*pedagogy*) ikiwemo mafunzo kwa vitendo kwa muda wa wiki 16.

Walimu wanaofundisha ngazi ya Sekondari pia wamegawanywa katika makundi mawili; kundi moja linaandaliwa katika vyuo vya ualimu na kundi la pili linaandaliwa katika vyuo vya elimu ya juu. Vyuo vya ualimu vinaandaa walimu wa Stashahada kwa muda wa miaka miwili na huchukua wahitimu wa Kidato cha Sita. Stashahada hiyo inajumuisha mafunzo ya maudhui ya masomo mawili kati ya matatu waliyochukua wakiwa Kidato cha Tano na Sita na masomo ya ualimu. Vilevile, Stashahada hiyo inaweza kuchukuliwa na wahitimu wa Kidato cha Nne kwa muda wa miaka mitatu na inajumuisha masomo ya Kidato cha Tano na Sita pamoja na mafunzo ya ualimu. Kama ilivyo kwa walimu tarajali wa Astashahada,



Taarifa ya Kamati Final.indd 43 08/05/2023 15:04

wale wa Stashahada pia huchukua mafunzo kwa vitendo yanayodumu kwa muda wa wiki 16 kabla hawajahitimu. Walimu wa Stashahada wanaandaliwa kufundisha Kidato cha Kwanza hadi cha Pili.

Kundi la mwisho la walimu linajumuisha wale wanaotoka katika vyuo vya elimu ya juu ambavyo huchukua wahitimu wa Kidato cha Sita na kuwapatia mafunzo ya Shahada ya Elimu. Shahada hiyo inajumuisha mafunzo ya maudhui ya masomo mawili (2), ualimu na mafunzo kwa vitendo kwa muda wa wiki 16. Walimu hawa wameandaliwa kufundisha ngazi zote za elimu ya sekondari na vyuo vya ualimu. Vilevile, kuna programu za mafunzo ya ualimu wa Elimu ya Awali na Msingi katika ngazi ya Shahada. Aidha, wahitimu wa elimu ya juu ambao hawakuchukua Shahada ya Elimu wanaweza kuandaliwa kuwa walimu kupitia mafunzo ya mwaka mmoja (1) ya Stashahada ya Uzamili katika Elimu (*Postgraduate Diploma in Education*).

Mfumo wa uandaaji wa walimu nchini unafanana kwa kiasi kikubwa na ule wa baadhi ya nchi za Afrika. Kwa mfano, nchini Kenya walimu wa shule za msingi ni wahitimu wa stashahada (*Diploma in Primary Education*) ambayo hutolewa kwa wahitimu wa Kidato cha Nne wenye ufaulu wa wastani wa C na hudumu kwa muda wa miaka mitatu (3). Masomo yanayofundishwa ni maudhui ya masomo, ualimu na mafunzo kwa vitendo yanayodumu kwa miezi mitatu (3). Walimu wa elimu ya msingi huandaliwa pia katika vyuo vya elimu ya juu ambapo hutunukiwa shahada ya ualimu wa elimu ya msingi.

Walimu wa Elimu ya Awali na wale wa Elimu Maalumu huandaliwa kupitia programu za mafunzo kazini ambazo hutolewa kwa walimu wa kawaida na huchukua muda wa miaka miwili (2) ambapo wahitimu hutunukiwa Stashahada. Walimu wa Elimu ya Awali, pia wanaweza kuandaliwa moja kwa moja baada ya kuhitimu Kidato cha Nne kwa wastani wa ufaulu wa C.

Walimu wa sekondari huandaliwa kupitia mifumo miwili. Mfumo wa kwanza ni kwa kupitia stashahada inayotolewa kwa wahitimu wa Kidato cha Nne wenye wastani wa ufaulu wa $C^{+}$. Stashahada hiyo huchukua muda wa miaka mitatu na hujumuisha maudhui katika masomo, ualimu na mafunzo kwa vitendo yanayodumu kwa miezi mitatu. Mfumo wa pili ni kupitia vyuo vikuu ambapo walimu tarajali huchukua mafunzo ya shahada ya elimu yanayodumu miaka minne. Vilevile, kuna mfumo wa kuandaa walimu wa Elimu ya Amali ambapo



Taarifa ya Kamati Final.indd 44 08/05/2023 15:04

wahitimu wa stashahada ya ufundi sanifu hupewa mafunzo ya ualimu.
Nchini Ghana, walimu huandaliwa kupitia mifumo miwili. Mfumo wa kwanza unaandaa walimu wenye stashahada ambao hufundisha kuanzia ngazi ya Elimu ya Awali hadi Sekondari Hatua ya Chini. Mwalimu tarajali anahitaji kuwa amepata ufaulu mzuri katika mtihani wa kumaliza elimu inayolingana na Kidato cha Sita cha Tanzania. Mafunzo haya huchukua muda wa miaka mitatu na yanajumuisha masomo ya kufundisha, ualimu na mafunzo kwa vitendo. Walimu wanaofundisha sekondari ngazi ya juu huandaliwa katika vyuo vya elimu ya juu na hutunukiwa shahada ya ualimu inayodumu kwa muda wa miaka minne. Walimu wote tarajali hulazimika kufanya kazi chini ya uangalizi (*internship*) kwa muda wa mwaka mmoja kabla hawajapewa leseni ya kufundisha. Hata hivyo, Ghana imeweka utaratibu wa kuhakikisha kuwa walimu wote ni wahitimu wa shahada ya elimu ya juu.

Nchini Zambia, pia kuna njia mbili za kuandaa walimu. Njia ya kwanza huandaa walimu wa stashahada ambao hufundisha kuanzia ngazi ya Elimu ya Awali hadi Sekondari Hatua ya Chini. Hata hivyo, Zambia iko mbioni kufuta walimu wa stashahada kufundisha katika ngazi ya sekondari. Mwalimu tarajali anahitaji kuwa amemaliza elimu inayolingana na ya Kidato cha Nne cha Tanzania na kufaulu masomo ya Kiingereza na Hisabati. Aidha, mwalimu tarajali anahitaji kufaulu mtihani wa kujiunga na chuo cha ualimu husika. Wahitimu hutunukiwa stashahada ya ualimu inayotolewa kwa muda wa miaka mitatu na mafunzo yanajumuisha maudhui ya masomo na ualimu.

Njia ya pili ni kwa kupitia vyuo vya elimu ya juu ambapo mwalimu tarajali huchukua shahada ya elimu ya ualimu inayodumu kwa muda wa miaka minne na inajumuisha mafunzo ya maudhui ya masomo na ualimu. Njia hii huandaa walimu kwa ajili ya kufundisha katika ngazi ya Elimu ya Msingi na Sekondari. Kabla ya kuruhusiwa kufundisha, mwalimu tarajali lazima apate leseni ya kufundishia inayotolewa na Baraza la Ualimu la Zambia (*Teaching Council of Zambia*) ambayo lazima ihuishwe kila baada ya miaka mitatu. Aidha, leseni isipohuishwa ndani ya miezi mitatu hufutwa. Vyuo vyote vya elimu nchini Zambia vimeshikizwa kwenye Chuo Kikuu cha Zambia kwa ajili ya uthibiti ubora.

Nchini Rwanda, walimu huandaliwa kupitia njia kuu mbili. Njia ya kwanza huandaa walimu wa elimu ya awali na msingi kupitia vyuo vya ualimu. Mafunzo huchukua muda wa miaka mitatu na hujumuisha maudhui ya masomo katika


Taarifa ya Kamati Final.indd 45 08/05/2023 15:04

michepuo ya Elimu ya Awali, Sayansi na Hisabati, Lugha na Sayansi ya Jamii. Aidha, walimu tarajali hufundishwa elimu ya ualimu na mafunzo kwa vitendo yanayodumu kwa muda wa miezi mitatu kabla hawajahitimu. Ili kujiunga na mafunzo haya, mwanafunzi anahitaji kuwa amehitimu elimu inayolingana na Kidato cha Nne cha Tanzania. Njia ya pili ya kuandaa walimu ni kwa kupitia vyuo vya elimu ya juu ambapo wahitimu wa elimu inayolingana na elimu ya Kidato cha Sita cha Tanzania huchukua shahada za ualimu. Mafunzo haya hujumuisha maudhui ya masomo, elimu ya ualimu na mafunzo kwa vitendo yanayodumu muda wa miezi sita kabla ya kuhitimu. Wahitimu wa mafunzo haya hufundisha katika shule za sekondari kwa wale waliojiunga moja kwa moja toka shuleni. Wahitimu waliojiunga katika vyuo vikuu wakitoka kazini, hurudi huko huko baada ya kuhitimu.

Nchini Mauritius, walimu wa elimu ya msingi huandaliwa kwa kupitia mafunzo ya stashahada yanayotolewa kwa wahitimu wa elimu inayolingana na Kidato cha Sita cha Tanzania. Mafunzo hayo hudumu kwa muda wa miaka miwili na yanajumuisha maudhui ya masomo, elimu ya ualimu na mafunzo kwa vitendo. Walimu wa elimu ya sekondari huwa ni wahitimu wa shahada za ualimu zinazotolewa na vyuo vya elimu ya juu au wahitimu wa elimu inayolingana na Kidato cha Sita cha Tanzania waliokamilisha mafunzo ya miaka mitatu yanayopelekea kutolewa kwa stashahada ya ualimu. Wahitimu wa elimu ya juu ambao hawajajifunza elimu ya ualimu wanaweza kupewa leseni ya kufundisha baada ya kuhitimu mafunzo maalumu ya wiki 15 yanayojumuisha misingi na mbinu za ualimu ikifuatiwa na wiki mbili ya mafunzo kwa vitendo shuleni.

Nchini Cameroon, walimu huandaliwa kupitia aina tatu za mafunzo. Katika mafunzo yote, walimu tarajali hujifunza maudhui ya masomo watakayoenda kufundisha, elimu ya ualimu na mafunzo kwa vitendo yanayodumu kwa wiki 24. Vilevile, baada ya kuhitimu walimu tarajali hufanya kazi chini ya uangalizi kwa muda wa kati ya wiki sita mpaka nane kabla ya kupewa leseni ya kufundishia. Kwa walimu wa elimu ya awali na msingi, mafunzo ya ualimu hutolewa kwa kipindi cha miaka mitatu kwa wahitimu wa shule ya msingi wenye ufaulu wa daraja C katika masomo yote. Vilevile, mafunzo haya hutolewa kwa muda wa miaka miwili kwa wahitimu wa elimu inayolingana na elimu ya Kidato cha Nne cha Tanzania. Wahitimu wote hawa hutunukiwa stashahada ya ualimu.

Aidha, walimu wanaondaliwa kufundisha katika shule za sekondari hatua ya chini ni wahitimu wa elimu inayolingana na Kidato cha Sita cha Tanzania na hupewa

mafunzo ya muda wa miaka mitatu na kutunukiwa stashahada. Mafunzo kwa ajili ya kuwaandaa walimu watakaofundisha sekondari hatua ya juu huandaliwa katika vyuo vya elimu ya juu baada ya kuhitimu elimu inayolingana na Kidato cha Sita cha Tanzania kwa ufaulu wa daraja C katika masomo mawili.


Nchini Afrika Kusini, walimu huandaliwa kupitia mifumo miwili. Mfumo wa kwanza hupokea wahitimu wa elimu inayolingana na Kidato cha Sita cha Tanzania na wanapata mafunzo ya ualimu kwa muda wa miaka minne katika vyuo vya elimu ya juu. Mfumo huu hujumuisha mafunzo sambamba ya maudhui ya masomo na elimu ya ualimu na wahitimu hutunukiwa shahada. Mfumo wa pili hupokea wahitimu wa elimu ya shahada ya kwanza ya elimu ya juu na kuwapatia mafunzo ya ualimu ya mwaka mmoja na kutunikiwa Stashahada ya Uzamili katika Elimu (*Postgraduate Diploma in Education*). Baada ya kuhitimu, walimu wote hutakiwa kupewa leseni na Baraza la Walimu la Afrika Kusini (*South African Council for Educators*) kabla hawajaruhusiwa kufundisha.

## 8.3 Mapendekezo ya Mfumo wa Elimu ya Ualimu Nchini Tanzania

Ingawa katika nchi nyingi zilizoendelea (nchi za OECD, Thailand, Hong Kong n.k), kiwango cha chini cha elimu inayohitajika kujiunga na mafunzo ya ualimu ni shahada ya elimu ya juu, katika nchi nyingi za Kiafrika walimu tarajali wana elimu kuanzia ngazi ya msingi (Cameroon), sekondari ya chini (Zambia, Kenya, Tanzania), sekondari ya juu (Rwanda) na elimu ya juu (Ghana, Afrika Kusini). Hata hivyo, nchi nyingi za Kiafrika zipo katika mchakato wa kuondokana na utaratibu wa kuandaa walimu wenye kiwango cha elimu chini ya ngazi ya sekondari hatua ya juu. Hii ni kwa sababu, tafiti mbalimbali zimeonesha kwamba ubora wa mwalimu unategemea sana kiwango cha elimu alichopata kabla hajajiunga na mafunzo ya ualimu. Kwa mantiki hiyo, na pia kwa kuzingatia maoni ya wadau, Kamati inapendekeza kwamba ngazi ya chini ya elimu kwa mwalimu tarajali iwe elimu ya Sekondari Hatua ya Juu. Hii ina maana kwamba, mafunzo ya astashahada ya ualimu kwa wahitimu wa Kidato cha Nne yafutwe. Badala yake inapendekezwa kuanzishwa kwa programu za Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Awali, Ualimu wa Elimu ya Msingi na Ualimu wa Elimu Maalumu.

Aidha, Kamati inapendekeza kwamba Stashahada zote za Ualimu zitolewe kwa muda wa miaka miwili na zipokee wahitimu kutoka Kidato cha Sita. Sababu ya mapendekezo hayo ni kwamba wahitimu wa Kidato cha Sita wameiva zaidi kitaaluma na hivyo mafunzo yao yatajikita katika kujifunza utalaamu wa ualimu


Taarifa ya Kamati Final.indd 47 08/05/2023 15:04




**Kielelezo Na. 5:** *Muundo Pendekezwa wa Elimu ya Ualimu*

badala ya masomo ya taaluma kama ilivyokuwa awali. Pendekezo hili linafuta ulazima wa kuongeza muda wa mafunzo ya ualimu kutoka miaka miwili hadi mitatu kama ilivyopendekezwa na wadau. Vilevile, inapendekezwa kwamba walimu waliopitia mafunzo haya wafundishe masomo mawili kati ya matatu waliyoyasoma katika tahasusi na ambayo wamejifunza mbinu za kuyafundishia.

Uzoefu kutoka nchi nyingine unaonesha wimbi la kuondokana na walimu wasio na shahada ya elimu ya juu. Kwa sababu hiyo, na kwa kuzingatia maoni ya wadau, Kamati inapendekeza kufuta stashahada ya ualimu wa sekondari na kufanya walimu wote wa ngazi hii wawe na shahada ya elimu. Aidha, Kamati inapendekeza kwamba, vyuo vya ualimu ambavyo kwa sasa vinatoa mafunzo ya stashahada ya ualimu wa sekondari vitumike kama vituo vya kutoa mafunzo endelevu kwa walimu (*continuous professional development*).

Ili kuweza kupata walimu wa Sekondari Hatua ya Chini kwa ajili ya Mkondo wa Elimu ya Amali, Kamati inapendekeza kuwe na programu ya Stashahada ya Uzamili katika Elimu itakayotolewa kwa wahitimu wa Shahada za elimu ya juu katika fani mbalimbali za Elimu ya Amali. Programu hii itajikita kwenye mbinu za ufundishaji na masomo ya ualimu tu. Ili kuhakikisha kwamba ufundishaji wa elimu ya amali unajumuisha uwiano stahiki baina ya mafunzo ya nadharia na yale ya vitendo, Kamati inapendekeza kwamba pamoja na kuandaa walimu wa elimu ya amali, waandaliwe pia wakufunzi wa karakana (*workshop instructors*) watakaosaidia kuendesha mafunzo kwa vitendo katika karakana/maabara. Karakana hizi zitatumika kuwawezesha wanafunzi kutafsiri kwa vitendo mafunzo ya kinadharia waliyopata darasani kwa msaada wa wakufunzi waliobobea katika fani husika. Inapendekezwa kuwa wakufunzi hawa waandaliwe kupitia programu ya Astashahada Maalumu ya Elimu ya Ualimu itakayotolewa kwa muda wa miezi sita kwa wahitimu wa elimu ya amali ngazi ya tatu (NVA III). Programu hii itajikita kwenye mbinu za ufundishaji na masomo ya ualimu tu.

Aidha, ili kuwa na suluhisho la kudumu kuhusu walimu wa mkondo wa Elimu ya Amali, Kamati inapendekeza kwamba vyuo vya elimu ya juu vianzishe programu za fani mbalimbali za elimu ya amali na ualimu kama vile Uhandisi na Ualimu, Sanaa Bunifu na Ualimu, Urembo na Ualimu, Uvuvi na Ualimu na kadhalika. Muundo pendekezwa wa elimu ya ualimu umeoneshwa kwenye Kielelezo Na. 5.



Taarifa ya Kamati Final.indd 49 08/05/2023 15:05

### 8.3.1 Mafunzo kwa Vitendo

Mafunzo kwa vitendo yamejumuishwa katika programu za uandaaji wa walimu kuanzia ngazi ya astahashada hadi shahada ya kwanza. Katika ngazi hizo zote, mafunzo kwa vitendo yanafanyika nje ya vyuo kwa muda wa wiki nane kwa mwaka wa kwanza na wa pili. Aidha, walimu tarajali wanatakiwa kufanya mazoezi ya kufundisha wakiwa vyuoni na katika shule zilizo karibu na vyuo vyao ingawa utekelezaji wake ni hafifu. Mafunzo nje ya vyuo hufanyika chini ya uangalizi wa vituo vya mafunzo na vyuo husika. Walimu tarajali hufanyiwa tathmini na wasimamizi wao katika vituo vya mafunzo kwa kushirikiana na wakufunzi kutoka vyuoni. Hata hivyo, mafunzo hayo yamegubikwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kurundikana kwa walimu tarajali katika shule moja na hivyo kupelekea kutopata muda wala usimamizi wa kutosha kufanya mazoezi, kutofanyika kwa muda uliopangwa, usimamizi hafifu na utoro. Changamoto hizi zimeathiri kwa kiasi kikubwa ufanisi wa mafunzo hayo na hivyo kuathiri ubora wa wahitimu.

Kamati inatambua umuhimu wa mafunzo kwa vitendo katika kujenga umahiri na weledi wa walimu tarajali. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba mfumo tulionao sasa unashindwa kutekeleza malengo hayo kwa ufanisi. Kwa sababu hiyo, Kamati inapendekeza kurekebisha mfumo wa uendeshaji wa mafunzo kwa vitendo kwa kusisitiza zaidi mafunzo endelevu kwa mwalimu tarajali anapokuwa chuoni na kwa kupitia shule zilizo jirani na vyuo. Lengo kuu la mafunzo hayo ni kutafsiri nadharia wanazojifunza darasani kwa vitendo kama vile haiba, maandalizi ya somo, kutumia mbinu za kufundishia, kuandaa na kutumia vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kutathmini wanafunzi. Vitendo vyote hivyo vitafanyika chini ya uangalizi wa karibu wa wakufunzi wao kwa lengo la kuwapatia mrejesho utakaowawezesha kuboresha umahiri wao darasani.

## 8.4 Weledi, Hadhi na Motisha kwa Walimu

Kama ilivyoelezwa awali, ni dhahiri kwamba ili mitaala itekelezwe kwa ufanisi, ni lazima kuwe na walimu wa kutosha wenye weledi, maadili na ari stahiki. Hii ina maana kwamba, kuna umuhimu wa kuwavutia wahitimu wenye ufaulu wa juu kujiunga na fani ya ualimu kwa kuboresha hadhi, maslahi, motisha na mazingira ya kazi kwa walimu. Utaratibu huu umetumiwa kwa ufanisi na nchi kadhaa duniani ikiwemo Rwanda na Peru. Kwa sababu hiyo, ili kuiongezea hadhi fani ya ualimu na kuifanya iweze kuwavutia wahitimu waliofaulu vizuri



RASIMU

Taarifa ya Kamati Final.indd 50 08/05/2023 15:05

kama wadau wengi walivyopendekeza, Kamati inapendekeza kwamba serikali iboreshe maslahi na mazingira ya kazi ya walimu. Sambamba na hilo, serikali iandae utaratibu wa kuwalipa posho maalumu walimu wanaofundisha katika mazingira magumu kama njia ya kuwamotisha na kufanya wabaki katika vituo vyao vya kazi. Vilevile, Kamati inapendekeza kwamba muundo wa utumishi wa walimu uboreshwe kwa kuufanya uzingatie ufanisi wa utendaji wa kila siku wa mwalimu katika kupanda madaraja (*performance based promotion*).

Kama ilivyopendekezwa na wadau, Kamati inapendekeza kwamba Sheria Na. 6 ya mwaka 2018 iliyoanzisha Bodi ya Usajili wa Walimu Tanzania itekelezwe haraka ili Bodi hiyo iweze kusimamia kikamilifu maadili na weledi wa walimu kama ilivyo kwenye tasnia nyingine. Bodi hiyo iwe na mamlaka ya kusajili na kusimamia elimu endelevu ya walimu (*continuous professional development*) na kuhakikisha kwamba walimu wanaoendelea na kazi ni wale tu wenye sifa na maadili stahiki. Utaratibu wa kusajili walimu umetumiwa kwa ufanisi na baadhi ya nchi ikiwemo Zambia, Afrika Kusini, Ghana, Kenya na nchi zote za OECD.

Ili kuimarisha umahiri na weledi wa walimu wachanga, Kamati inakubaliana na maoni ya wadau na kupendekeza wahitimu wote wa programu za ualimu wafanye kazi chini ya uangalizi wa walimu wazoefu (*internship*) kwa kipindi cha mwaka mmoja kabla hawajapewa leseni ya kufundisha. Hivyo basi, Kamati inapendekeza kwamba serikali kupitia wizara inayohusika na elimu iandae mwongozo wa namna ya kusimamia mafunzo haya. Nchi nyingine kama vile Zambia, Ghana na Kenya zimeanzisha utaratibu kama huu kwa ufanisi.

Ili kutekeleza kwa ufanisi mitaala pendekezwa ya ualimu, ni muhimu kuwa na wakufunzi wenye umahiri na weledi stahiki. Kwa kuzingatia maudhui yaliyomo katika mtaala wa stashahada ya ualimu, Kamati inapendekeza kwamba, wakufunzi wa vyuo vya ualimu wawe na angalau Shahada ya Umahiri katika masomo ya ualimu na uzoefu wa kufundisha usiopungua miaka miwili katika ngazi husika. Hii ina maana kwamba, kwa mfano, mkufunzi anayetekeleza mafunzo ya ualimu wa Elimu ya Msingi anapaswa kuwa na uzoefu wa kufundisha katika shule ya msingi kwa muda wa miaka miwili au zaidi. Sifa hizi zitamwezesha kuwa mkufunzi bora kwani atakuwa anafahamu mazingira halisi ambayo mwalimu tarajali atakwenda kufanya kazi.


Taarifa ya Kamati Final.indd 51 08/05/2023 15:05

## 8.5 Mitaala ya Elimu ya Ualimu

Mabadiliko ya mitaala yanayopendekezwa katika Ripoti hii yanalenga kubadili namna ufundishaji na ujifunzaji unavyofanyika. Mabadiliko hayo yanajumuisha kumfanya mwanafunzi awe kitovu cha ujifunzaji (*student centred learning)*, matumizi ya TEHAMA na teknolojia mbalimbali saidizi, uchopekaji wa masuala mtambuka katika masomo bebezi, kuzingatia Stadi za Karne ya 21 na dhana ya upimaji kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri. Mfumo wetu wa sasa wa kuandaa walimu hauwajengei uwezo wa kumfanya mwanafunzi awe kitovu cha ujifunzaji na wala haumtayarishi kufundisha kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri. Aidha, mfumo wetu haumtayarishi mwalimu kuweza kufundisha na kupima maendeleo ya mwanafunzi kwa kuzingatia Stadi za Karne ya 21. Kwa maana hiyo, ni lazima mabadiliko ya mitaala ya elimu ya ualimu yaakisi mabadiliko yanayopendekezwa katika mitaala ya shule.

Kwa ujumla uandaaji wa mitaala ya elimu ya ualimu ujikite katika kujenga umahiri wa mwalimu tarajali katika maeneo ya msingi yafuatayo:

(a) Maudhui ya masomo anayofundisha (*subject content mastery*).

(b) Usimamizi wa ujifunzaji na ufundishaji (*classroom management*).

(c) Mbinu za kufundishia (*didactics*).

(d) Mbinu za upimaji (*assessment*) ili kubaini mafanikio na kuboresha ujifunzaji na ufundishaji.

Misingi hii itatafsiriwa katika mitaala kama ifuatavyo:

*(i) Umahiri katika masomo anayofundisha*

Mwalimu tarajali atapata umahiri wa masomo anatakayofundisha kupitia elimu yake kabla hajajiunga na mafunzo ya ualimu.

*(ii) Usimamizi wa ujifunzaji na ufundishaji*

Umahiri katika usimamizi wa darasa utapatikana kupitia masomo kama saikolojia ya elimu kwa rika husika (*grade-appropriate educational psychology*), sosholojia ya elimu, mbinu za kuwasiliana kwa rika husika, mafunzo ya maadili na weledi (*professionalism and ethics*); na uwezo wa kuendesha mafunzo (*instructional leadership*)

*(iii)* *Mbinu za kufundishia*

Mbinu za kufundishia zitapatikana kupitia mafunzo ya mbinu maalumu kwa masomo yake na zitajumuisha matumizi ya TEHAMA, teknolojia nyingine saidizi na ufaraguzi katika ufundishaji na ujifunzaji, uchopekaji wa masuala mtambuka katika masomo bebezi na uelewa wa masuala jumuishi katika ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, mbinu hizo zitamwezesha mwalimu tarajali kumjengea mwanafunzi umahiri katika Stadi za Karne ya 21 ikiwemo uwezo wa kuwasiliana, kushirikiana, fikra tunduizi na utatuzi wa matatizo. Pia, kwa kuzingatia mtaala wa ujenzi wa umahiri, inabidi mwalimu tarajali afundishwe mbinu za kumjengea mwanafunzi maarifa, stadi na mwelekeo.

Uzoefu umeonesha kwamba watoto wadogo wanajifunza vizuri zaidi kupitia michezo. Hivyo, ni lazima kumjengea mwalimu tarajali wa madarasa ya awali (elimu ya awali hadi darasa la pili) umahiri wa kutumia michezo kama nyenzo muhimu ya ufundishaji na ujifunzaji. Kwa kuzingatia hali halisi ya mazingira yetu, ambapo uwiano kati ya idadi ya wanafunzi kwa kila mwalimu unazidi viwango tulivyojiwekea, ni mhimu pia mwalimu tarajali ajengewe umahiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa madarasa makubwa kwa ufanisi.

Ili kuwezesha ufanisi katika mawasiliano wakati wa ufundishaji na ujifunzaji, Kamati inapendekeza kwamba mwalimu tarajali afundishwe katika lugha ambayo atafundishia. Aidha, Kamati inapendekeza kuanzisha somo jipya la lazima linalotilia mkazo kumjengea mwalimu uwezo wa kuwasiliana kitaalamu *(professional communication for teachers*) katika lugha atakayofundishia.

*(iv)* *Mbinu za upimaji*

Mwalimu tarajali atafundishwa mbinu za upimaji endelevu na tamati unaozingatia ujenzi wa umahiri pamoja na Stadi za Karne ya 21 ikiwemo kuwajengea wanafunzi ubunifu, fikra tunduizi na uwezo wa kutatua matatizo.

Kwa kuzingatia mabadiliko ya mitaala ya shule yanayopendekezwa katika Ripoti hii na umahiri wa msingi wa elimu ya ualimu kama ilivyotafsiriwa hapo juu,



RASIMU

Taarifa ya Kamati Final.indd 53 08/05/2023 15:05

Kamati inapendekeza kuboresha lengo kuu na malengo mahususi ya elimu ya ualimu kama ilivyoainishwa katika Sehemu 8.6 ya Ripoti hii. Aidha, rasimu za mitaala zinazoakisi malengo na umahiri huo zimeoneshwa katika Viambatisho Na. 5 na 6.

## 8.6 Malengo ya Elimu ya Ualimu

### 8.6.1 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu

Kumwandaa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ujifunzaji na ufundishaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, na kijamii ili kumjenga Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo.

### 8.6.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu

Malengo ya Elimu ya Ualimu ni kumwezesha mwalimu tarajali:

(i) Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha, na misingi ya ualimu.

(ii) Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia.

(iii) Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri.

(iv) Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi.

(v) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji.

(vi) Kukuza utambuzi wa awali wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki.

(vii) Kuimarisha matumizi ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji.

(viii) Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (*classroom-based action research*).

## 8.7 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ualimu

Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu unalenga kumwezesha mwalimu tarajali:

(i) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji na ujifunzaji.

(ii) Kumudu mbinu za kufundishia na kujifunzia.



Taarifa ya Kamati Final.indd 54 08/05/2023 15:05

(iii) Kumudu mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri.

(iv) Kumudu mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi.

(v) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji.

(vi) Kutambua mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki.

(vii) Kutumia lugha husika kwa ufasaha katika ufundishaji na ujifunzaji.

(viii) Kutumia stadi za uongozi katika taaluma (*instructional leadership*).

(ix) Kumudu stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (*classroom-based action research*).

### 8.7.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Stashahada ya Ualimu

Katika ngazi ya Stashahada ya Ualimu mwalimu tarajali atakuwa na maeneo ya kujifunza na masomo kama ilivyobainishwa katika Jedwali Na. 8, 9 na 10.

**Jedwali Na. 8:** Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Stashahada ya Ualimu (Elimu ya Awali)

| Na. | Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo |
|---|---|---|
| 1. | Misingi ya Kinadharia | Falsafa na Maadili ya Ualimu |
| | | Saikolojia na Sosholojia ya Elimu |
| | | Mitaala na Ufundishaji |
| | | Upimaji na Tathamini |
| 2. | Ualimu kwa Vitendo | Ualimu kwa Vitendo |
| 3. | Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji | Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo husika |
| 4. | Masomo ya Jumla | Elimu Jumuishi |
| 5. | Lugha na Mawasiliano | Mawasiliano ya Kitaaluma kwa Walimu |



Taarifa ya Kamati Final.indd 55 08/05/2023 15:05

**Jedwali Na. 9:** Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Stashahada ya Ualimu (Elimu ya Msingi)

| Na. | Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo |
|---|---|---|
| 1. | Misingi ya Kinadharia | Falsafa na Maadili ya Ualimu |
| | | Saikolojia na Sosholojia ya Elimu |
| | | Mitaala na Ufundishaji |
| | | Upimaji na Tathamini |
| 2. | Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji* | Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa masomo ya Lugha |
| | | Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa Sayansi |
| | | Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa Hisabati |
| | | Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa Sayansi Jamii |
| | | Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa Sanaa na Michezo |
| | | Ualimu kwa Vitendo |
| 3. | Masomo ya Jumla | Elimu Jumuishi |
| 4. | Lugha na Mawasiliano | Mawasiliano ya Kitaaluma kwa Walimu |

** Mwalimu tarajali atachagua kujifunza mbinu za masomo mawili tu kati ya matatu aliyochukua katika tahasusi yake ya Kidato cha Tano na cha Sita.*

**Jedwali Na. 10:** Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Stashahada ya Ualimu (Elimu Maalumu)

| Na. | Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo |
|---|---|---|
| 1. | Misingi ya Kinadharia | Falsafa na Maadili ya Ualimu |
| | | Saikolojia na Sosholojia ya Elimu |
| | | Mitaala na Ufundishaji |
| | | Upimaji na Tathamini |
| 2. | Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji* | Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni |
| | | Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji kwa mwanafunzi mwenye uziwi |



Taarifa ya Kamati Final.indd 56 08/05/2023 15:05

| Na. | Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo |
|---|---|---|
| | | Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona |
| | | Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili |
| | | Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji kwa mwanafunzi mwenye usonji<br>Ualimu kwa Vitendo |
| 3. | Masomo ya Jumla | Elimu Jumuishi |
| 4. | Lugha na Mawasiliano | Mawasiliano ya Kitaaluma kwa Walimu |

** Mwalimu tarajali atachagua kujifunza mbinu za fani mbili tu za elimu maalumu. Aidha, atajifunza mbinu za kufundisha somo moja kutoka katika mtaala wa elimu ya awali au elimu ya msingi.*

Maelezo zaidi kuhusu umahiri mkuu na umahiri mahususi kwa kila somo yanapatikana katika Kiambatisho Na. 5.

## 8.8 Umahiri wa Jumla wa Astashahada ya Ukufunzi wa Karakana/ Maabara (Elimu ya Amali)

Mafunzo ya Astashahada Maalumu ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini – Amali unalenga kumwezesha mkufunzi tarajali:

(i) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji kwa vitendo wa fani za elimu ya amali.

(ii) Kumudu mbinu za kufundisha kwa vitendo fani za elimu ya amali.

(iii) Kumtambua mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji kwa vitendo na kutoa afua stahiki.

(iv) Kumudu misingi ya usimamizi wa karakana/maabara.

### 8.8.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Astashahada ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara (Elimu ya Amali)

Katika ngazi ya Astashahada Maalumu ya Ualimu wa Elimu ya Amali, mwalimu tarajali atakuwa na maeneo ya kujifunza na masomo kama ilivyobainishwa katika Jedwali Na. 11.



Taarifa ya Kamati Final.indd 57 08/05/2023 15:05

**Jedwali Na. 11:** Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Astashahada ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara (Elimu ya Amali)

| Na. | Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo |
|---|---|---|
| 1. | Ukufunzi wa Karakana/Maabara katika Elimu ya Amali | Misingi ya Ukufunzi wa Karakana/ Maabara katika Elimu ya Amali |
| 2. | Misingi ya Usimamizi wa Karakana/ Maabara | Usimamizi wa Karakana/Maabara |

Maelezo zaidi kuhusu umahiri mkuu na umahiri mahususi kwa kila somo yanapatikana katika Kiambatisho Na. 6.

## 8.9 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ni nyenzo muhimu inayomwezesha mwanafunzi kupenda kujifunza kwa ufanisi. Kiunzi cha Taifa cha Mitaala ya Elimumsingi na Ualimu cha mwaka 2019 kinasisitiza umuhimu wa matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazomshirikisha mwanafunzi. Katika muktadha wa mtaala wa ujenzi wa umahiri, ni muhimu kwa mwanafunzi kujenga umahiri unaokusudiwa kwa kutenda shughuli mbalimbali ndani na nje ya darasa. Hivyo basi, mbinu zinazotumika kufundishia na kujifunzia ziwe na tija katika kumwezesha mwanafunzi kujenga umahiri uliolengwa.
Kwa mantinki hiyo, Kamati inapendekeza kuboresha mfumo wa ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia mbinu zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji na mwalimu kuwa mwezeshaji. Mwalimu atumie mbinu zinazomshirikisha mwanafunzi katika tendo zima la ujifunzaji kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai (*diverse needs*), na uwezo wa mwanafunzi. Kwa ujumla, njia zinazopendekezwa kutumika katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ni shirikishi, zikiwemo zile zinazomwezesha mwanafunzi kufikiri na kutafakari. Vilevile, njia hizo zimwezeshe mwanafunzi kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo maktaba mtandao, machapisho na ripoti. Njia za kufundishia na kujifunzia zinazopendekezwa ni pamoja na ziara za kimasomo, kazi za vitendo, kazimradi, majadiliano, utafiti, majaribio ya kisayansi, na nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujenzi wa umahiri uliokusudiwa.

Aidha, katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu asiwe chanzo pekee cha maarifa na stadi mbalimbali badala yake awe mwezeshaji anayetoa uzoefu wa jambo ambalo mwanafunzi anajifunza. Mwanafunzi anapaswa kuwa



Taarifa ya Kamati Final.indd 58 08/05/2023 15:05

mtendaji mkuu katika mchakato wa kujifunza. Wazazi, walezi, wakuza mitaala, wataalamu wa afya na wataalamu wengine washirikishwe katika shughuli za ufundishaji na ujifunzaji.

Masuala mtambuka ni miongoni mwa mambo muhimu yaliyozingatiwa katika mitaala inayopendekezwa. Kamati inapendekeza kwamba masuala haya yafundishwe kwa kuyachopeka wakati wa vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji katika masomo mbalimbali yanayotambulika kama masomo bebezi kwa kuzingatia uhusiano wa suala mtambuka na somo bebezi. Mapendekezo ya mabadiliko ya mfumo wa ufundishaji na ujifunzaji yanalazimu kuimarisha programu za mafunzo ya ualimu vyuoni na kazini ili kuwajengea walimu uwezo wa kutumia mbinu muafaka za ufundishaji na ujifunzaji.

## 8.10 Upimaji na Tathmini ya Ujifunzaji na Ufundishaji

Upimaji katika elimu hufanyika kwa lengo la kujua maendeleo ya mwanafunzi kwa kile anachokijua, anachoweza kufanya, mabadiliko ya tabia na mwelekeo na kubaini changamoto ya mwanafunzi katika kujifunza ili kuzitafutia ufumbuzi. Aidha, upimaji huamsha ari ya mwanafunzi kujifunza zaidi na kuboresha ufundishaji.

Kama ilivyobainishwa katika *Sera ya Elimu na Mafunzo* ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023, kuna haja ya kuimarisha upimaji na tathmini ya maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma. Hivyo basi, Kamati inapendekeza kuboresha mfumo wa upimaji kwa kutumia vigezo vinavyotambulika vya upimaji wa maendeleo ya kila siku ya mwanafunzi na tathmini ya mwisho ya kukamilisha ngazi husika kwa kuzingatia mtaala wa ujenzi wa umahiri. Upimaji wa ndani ufanyike na kuratibiwa shuleni au chuoni sambamba na ufundishaji na ujifunzaji; na upimaji wa nje uratibiwe na kutekelezwa na mamlaka husika zikiwemo NECTA na NACTVET ili kuhakikisha uthabiti (*validity*) na kuaminika (*reliability*) kwa upimaji wa ndani.

Aidha, Kamati inapendekeza kwamba zana na mbinu za upimaji na tathmini ziwe zile zinazopima nadharia na vitendo zikiwemo bunguabongo, orodhahakiki, majaribio, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi, kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi. Zana na mbinu nyingine zinaweza kuwa majaribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya muhula na mtihani wa mwisho. Matumizi ya zana na mbinu hizi yatatofautiana kulingana



Taarifa ya Kamati Final.indd 59 08/05/2023 15:05

na sababu ya upimaji, aina na mahitaji ya somo, mahitaji anuai ya mwanafunzi, na umahiri unaokusudiwa kujengwa.

Kwa kuzingatia maoni ya wadau, wakiwemo wale wa Baraza la Mitihani la Tanzania, Kamati inapendekeza kwamba upimaji endelevu uchangie uzito usiopungua asilimia 30 ya upimaji wote. Aidha, inapendekezwa kwamba kwa tathmini ya kuhitimu Kidato cha Nne, mchango wa alama hizi utokane na Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Sita (7.5%), Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (7.5%), mtihani wa muhula wa mwisho wa Kidato cha Tatu (5%), kazimradi (*project*) inayofanyika mwishoni mwa Kidato cha Tatu (5%), na mtihani wa utamilifu (*mock*) wa Kidato cha Nne (5%). Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Sita na Kidato cha Pili umepewa uzito mkubwa kwa sababu unaandaliwa na kuratibiwa na Baraza la Mitihani la Tanzania, hivyo uthabiti (*validity*) na kuaminika (*reliability*) kwake ni kwa hali ya juu.

Kwa upande wa Sekondari Hatua ya Juu, Kamati inapendekeza kwamba upimaji endelevu utokane na alama za mtihani wa muhula wa kwanza wa Kidato cha Tano (5%), mtihani wa muhula wa pili wa Kidato cha Tano (5%), mtihani wa muhula wa kwanza wa Kidato cha Sita (5%), kazimradi (10%) na mtihani wa utamilifu (5%). Pia, Kamati inapendekeza kwamba upimaji wa masomo ya Elimu ya Amali ufanyike kwa kuzingatia sheria na taratibu za NACTVET.

Kwa Elimu ya Ualimu, Kamati inapendekeza kwamba upimaji endelevu utokane na alama za mitihani ya mihula (5%), kazimradi ya ufaraguzi (10%) na mafunzo kwa vitendo (45%). Upimaji tamati, ambao utabeba asilimia 40 ya upimaji wote, utaendelea kutolewa na Baraza la Mitihani Tanzania. Aidha, Kamati inapendekeza kwamba alama za mafunzo kwa vitendo zitokane na ufundishaji wa kuigiza (20%) na ufundishaji katika shule jirani (25%). Inapendekezwa mwalimu tarajali afaulu upimaji endelevu kwa angalau asilimia 50 na upimaji tamati kwa angalau kiwango hichohicho ili aweze kutunukiwa cheti. Endapo hatafaulu, mwalimu tarajali anaweza kurudia mitihani hiyo mara mbili ndani ya miaka mitatu.



Taarifa ya Kamati Final.indd 60 08/05/2023 15:05

# 9.0 Mikakati ya Utekelezaji

## 9.1 Utangulizi

Uzoefu kutoka nchi mbalimbali zilizotekeleza mabadiliko ya mitaala umeonesha umuhimu wa maandalizi ya kutosha ya rasilimali watu, miundombinu na vifaa vya mtaala kabla mtaala mpya haujatekelezwa. Mafanikio ya maandalizi hayo yanahitaji kwa kiasi kikubwa uwepo wa fedha za kutosha. Kwa upande wa rasilimali watu, utekelezaji utahitaji kuajiri walimu wa masomo mapya (kama vile Elimu ya Amali, Elimu ya Biashara, Chakula na Lishe, Sanaa Bunifu, Michezo, Sanaa Sanifu na Muziki) pamoja na kutoa mafunzo kazini kwa walimu na watekelezaji wote wa mitaala hiyo. Aidha, ni muhimu kuandaa na kuajiri walimu wapya ili kukabiliana na ongezeko la wanafunzi wa sekondari. Pia, itabidi kuandaa na kuajiri wakufunzi wa karakana kwa ajili ya mkondo wa elimu ya amali.

Kuhusu miundombinu, utekelezaji utahitaji ujenzi na/au ukarabati wa karakana na maabara kwa ajili ya elimu ya amali. Pia, itabidi kujenga madarasa, vyoo, maktaba na ofisi za walimu ili kukabiliana na ongezeko la walimu na wanafunzi wa sekondari. Aidha, ni muhimu kuandaa na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinavyokidhi mahitaji ya mitaala mipya kwa wakati. Vifaa hivyo ni pamoja na mihtasari ya masomo husika, vitabu vya kiada na ziada, kiongozi cha mwalimu na visaidizi vya kiteknolojia kama vile vishikwambi.

## 9.2 Mikakati ya Utekelezaji wa Mitaala Mipya

Uzoefu unaonesha kwamba utekelezaji wa mitaala mipya unaweza kuanza kwa kutumia mikakati mbalimbali. Mikakati hiyo ni pamoja na:

### 9.2.1. Utekelezaji Kuanza na Darasa Moja kwa Wakati Mmoja

Katika mkakati huu, utekelezaji wa mtaala mpya huanza na darasa moja katika ngazi moja ya elimu katika shule zote kwa wakati mmoja. Hususani, mkakati huu huanzia madarasa ya chini na kupanda kila mwaka katika madarasa yanayofuata *(bottom-up).* Mkakati huu unaruhusu ujenzi wa umahiri kimpangilio kuanzia madarasa ya chini kwenda madarasa ya juu. Aidha, mkakati huu una faida ya kutoa muda wa kutosha wa kufanya maandalizi ya utekelezaji, ikiwemo kutoa mafunzo kwa walimu na kuandaa vifaa vya mtaala kwa makundi kulingana na darasa linaloanza utekelezaji. Changamoto kubwa ya mkakati huu ni kuchukua



Taarifa ya Kamati Final.indd 61 08/05/2023 15:05

muda mrefu kukamilisha utekelezaji wa mzunguko wa mitaala hali ambayo inaweza kukatisha tamaa jamii kwa sababu haioni tija ya mabadiliko ya mitaala mapema. Katika baadhi ya nchi hali hii ilileta taharuki zilizotishia utekelezaji wa mabadiliko ya mitaala yaliyokusudiwa.

### 9.2.2. Utekelezaji katika Madarasa Yote kwa Pamoja

Katika mkakati huu, utekelezaji wa mtaala mpya huanza katika madarasa yote ya ngazi husika ya elimu kwa wakati mmoja. Mkakati huu huambatana na changamoto nyingi za utekelezaji, ikiwemo ugumu wa ujifunzaji wa baadhi ya maudhui kwa wanafunzi wa madarasa ya juu ambayo misingi yake hujengwa katika madarasa ya chini. Aidha, mkakati huu huhitaji umakini mkubwa katika maandalizi kwa sababu kazi zote za utekelezaji wa mtaala zitatakiwa kufanyika kwa wakati mmoja, ikiwemo mafunzo ya walimu wote, kuandaa miundombinu na kusambaza vifaa vya utekelezaji wa mtaala.

### 9.2.3. Utekelezaji kwa Pamoja katika Makundi ya Madarasa

Katika mkakati huu, utekelezaji wa mtaala mpya hufanyika kwa pamoja katika makundi ya madarasa *(clusters of grades)*. Kwa mfano, mtaala mpya unaweza kuanza kutekelezwa katika darasa la kwanza na pili katika mwaka wa kwanza na kufuatiwa na kundi la darasa la tatu hadi la sita katika mwaka wa pili. Mkakati huu hutumika zaidi kwenye ngazi za elimu zinazochukua muda mrefu ambapo utekelezaji kamili wa mtaala kwa darasa moja moja utachukua muda mrefu kukamilisha mzunguko.

Ingawa utekelezaji kwa makundi ya madarasa unasaidia kufikia utekelezaji kamili wa mtaala katika muda mfupi, mkakati huu husababisha changamoto ya ujifunzaji wa baadhi ya maudhui kwa wanafunzi wa madarasa ya juu ambayo misingi yake hujengwa katika madarasa ya chini.

### 9.2.4. Utekelezaji Kuanza na Darasa Moja Moja katika kila Kundi

Katika njia hii madarasa hugawanywa kimkakati katika makundi, kisha utekelezaji wa mtaala huanza na darasa la chini katika kila kundi. Kwa mfano, katika kundi la darasa la kwanza na la pili utekelezaji unaanza na darasa la kwanza na katika kundi la darasa la tatu hadi la sita utekelezaji unaanza na darasa la tatu. Baada ya hapo, utekelezaji unaendelea katika darasa linalofuata katika kila kundi mpaka kufikia madarasa yote. Faida ya mkakati huu ni kwamba unapunguza changamoto ya ujifunzaji wa baadhi ya maudhui kwa wanafunzi wa madarasa ya juu ambayo



Taarifa ya Kamati Final.indd 62 08/05/2023 15:05

misingi yake hujengwa katika madarasa ya chini. Aidha, mkakati huu unaruhusu kukamilisha mzunguko wa mtaala katika muda mfupi na kuruhusu maandalizi na maboresho kuendelea katika muda wote wa utekelezaji.

## 9.3 Mkakati Unaopendekezwa

Mabadiliko ya muundo na mitaala yanayopendekezwa katika Ripoti hii ni makubwa na kwa kiasi kikubwa yametokana na maoni ya wadau. Hii ina maana kwamba, jamii ina matarajio makubwa na inasubiri kwa shauku utekelezaji wa mabadiliko hayo. Hivyo, kuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba utekelezaji unakidhi matarajio na shauku hiyo ya jamii. Ili kuhakikisha hayo, utekelezaji unatakiwa ufanyike kwa umakini mkubwa na katika muda mfupi ili kuepusha jamii kupoteza shauku ya mabadiliko. Aidha, ili kufanya gharama ziwe himilivu *(avoid budgetary distress)* kuna umuhimu wa kutekeleza mabadiliko hayo hatua kwa hatua kwa kuzingatia matarajio na shauku ya jamii na uhalisia wa kibajeti. Kwa sababu hiyo, Kamati inapendekeza mkakati wa utekelezaji wa mitaala mipya kwa makundi ya madarasa kwa kuanza na darasa la chini katika kila kundi kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 12.

**Jedwali Na. 12:** Mkakati wa Utekelezaji wa Mitaala Mipya kwa Makundi ya Madarasa

| Kundi | Darasa la Kuanzia | Mwaka wa Kuanza Mzunguko | Mwaka wa Kukamilisha Mzunguko |
|---|---|---|---|
| Stashahada ya Ualimu (Elimu ya Amali ) | Mwaka wa 1 | 2024 | 2026 |
| Astashahada ya Ualimu(Elimu ya Amali) | Miezi 6 | 2024 | 2024 |
| Sekondari Hatua ya Juu (K5–6) | Kidato cha 5 | 2024 | 2026 |
| Sekondari Hatua ya Chini-Amali (K 1-4)* | Kidato cha 1 | 2024 (*Piloting*) | 2027 |
| Sekondari Hatua ya Chini-Amali (K 1-4)* | Kidato cha 1 | 2025 (*Actual Roll-out*) | 2028 |
| Sekondari Hatua ya Chini-Jumla (K 1-4)* | Kidato cha 1 | 2024 | 2027 |
| Elimu ya Msingi (Drs III-VI) | Darasa la III | 2024 | 2027 |
| Elimu ya Msingi (Drs I-II) | Darasa la I | 2024 | 2025 |
| Elimu ya Awali | Darasa la Awali | 2024 | 2024 |

**Wahitimu wote wa Elimu ya Msingi wataanza kujiunga na Sekondari Hatua ya Chini mwaka 2025*


Taarifa ya Kamati Final.indd 63 08/05/2023 15:05

Kulingana na mkakati huu, inapendekezwa kwamba katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji, mitaala mipya ianze na Darasa la Awali, Darasa la Kwanza, Darasa la Tatu, Kidato cha Kwanza na Kidato cha Tano. Kwa upande wa elimu ya ualimu, utekelelezaji utaanza na mwaka wa kwanza wa stashahada ya ualimu na astashahada maalumu ya wakufunzi wa karakana. Uchaguzi wa makundi hayo umezingatia muundo wa mitaala ya ngazi husika za elimu ambapo maudhui ya ngazi za awali, darasa la kwanza na la pili, darasa la tatu hadi la sita, kidato cha kwanza hadi cha nne na kidato cha tano na cha sita yanajitegemea kwa kiwango kikubwa.

Katika kidato cha kwanza utekelezaji wa mtaala mpya kwa mkondo wa elimu ya amali utaanza mwaka 2024 kwa majaribio (*piloting)* katika baadhi ya shule na fani ambazo hali ya miundombinu inaruhusu. Hii ni kwa sababu mkondo huu ni mpya na unahitaji maandalizi ya kutosha ya walimu, wakufunzi wa karakana, karakana na maabara. Kuanzia mwaka 2025, utekelezaji wa elimu ya amali utaendelea katika shule na fani nyingi zaidi na kupanuliwa kila mwaka hadi itakapofikia uwiano stahiki baina ya idadi ya wanafunzi wa elimu ya jumla na wale wa elimu ya amali mwaka 2030. Uwiano huo utategemea mahitaji halisi ya kiuchumi ya Taifa na utajumuisha uwiano wa idadi ya wanafunzi katika kila mkondo na katika kila fani ya amali.

Ili kupata muda wa kutosha wa maandalizi, inapendekezwa kwamba utekelezaji wa elimu ya lazima ya Sekondari Hatua ya Chini uanze mwaka 2025. Kuanza kwa utekelezaji wa mtaala mpya katika Darasa la Tatu mwaka 2024 kutasababisha kuwa na makundi mawili yatakayohitimu elimu ya msingi mwaka 2027. Hivyo basi, mwaka 2028 kutakuwa na makundi mawili (*double cohort*) ya wanafunzi wa Kidato cha Kwanza. Makundi haya yatahitimu Kidato cha Nne mwaka 2031.

Endapo utekelezaji utaanza mwaka 2024, mzunguko wa elimu ya awali utakamilika mwaka huo huo, ule wa darasa la kwanza na la pili utakamilika mwaka 2025 na wa darasa la tatu mpaka la sita utakamilika mwaka 2027. Kwa upande wa sekondari hatua ya chini elimu ya jumla, mzunguko utakamilika mwaka 2027, wakati ule wa kidato cha tano na cha sita utakamilika mwezi Mei 2026. Kwa upande wa sekondari hatua ya chini elimu ya amali, mzunguko utaanza mwaka 2025 na kukamilika mwaka 2028. Utekelezaji wa mitaala mipya ya elimu ya ualimu utaanza mwaka 2024 na kukamilika mwaka huohuo kwa astashahada maalumu ya ualimu wa amali na mwaka 2025 kwa stashahada ya


Taarifa ya Kamati Final.indd 64 08/05/2023 15:05

elimu ya ualimu. Kwa utaratibu huu, mzunguko wa utekelezaji wa mitaala yote hii utakamilika katika kipindi cha miaka minne. Katika muda wote wa utekelezaji kutakuwa na ufuatiliaji na tathmini ili kuboresha mitaala hiyo na vifaa vyake.

RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 65 08/05/2023 15:05

# 10.0 Muhtasari wa Mapendekezo Makuu

Mapendekezo yaliyopo katika Ripoti hii yanaweza kugawanywa katika sehemu kuu tatu: muundo wa elimu rasmi, mitaala na Elimu ya Ualimu.

## 10.1 Muundo wa Elimu Rasmi

(i) Elimu ya Awali itolewe kwa muda wa mwaka mmoja kwa watoto wa umri wa miaka mitano kama inavyoelekezwa na *Sera ya Elimu na Mafunzo* ya mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023.

(ii) Kwa kuzingatia hali halisi ya utoaji wa elimu hiyo kwa sasa, hususan upungufu mkubwa sana wa walimu wenye sifa stahiki waliopo shuleni na kwenye soko la ajira, inapendekezwa elimu hii isiwe ya lazima kwa sasa. Serikali iendelee kuweka mikakati mahususi ikiwemo kuandaa walimu mahiri wa Elimu ya Awali na miundo mbinu rafiki, fikivu na ya kutosha kabla ya kuamua kuifanya elimu hiyo kuwa ya lazima.

(iii) Muda wa Elimu ya Msingi upunguzwe kutoka miaka saba (7) hadi miaka sita (6) kama inavyoelekezwa na *Sera ya Elimu na Mafunzo* ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023. Aidha, umri wa kuanza Darasa la Kwanza uwe miaka sita (6) na ule wa kuanza Kidato cha Kwanza uwe miaka 12.

(iv) Muda wa Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini uendelee kuwa miaka minne (4) na ule wa Sekondari Hatua ya Juu pia uendelee kuwa miaka miwili (2).

(v) Kama inavyoelekezwa na *Sera ya Elimu na Mafunzo* ya mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023, elimu ya Msingi na ile ya Sekondari Hatua ya Chini ziwe za lazima hivyo kuifanya elimu ya lazima (*compulsory basic education*) kuwa miaka kumi (10).

(vi) Mfumo wa elimu unyumbuliwe kuanzia Kidato cha Kwanza kwa kuanzisha mikondo miwili, mmoja wa Elimu ya Jumla na mwingine wa Elimu ya Amali.

(vii) Kila shule ya Sekondari Hatua ya Chini iwe na mkondo wa Elimu ya Jumla na mkondo wa Elimu ya Amali. Ili kurahisisha uendeshaji, shule moja isiwe na zaidi ya fani mbili za Elimu ya Amali.

(viii) Wanafunzi wa mkondo wa Elimu ya Amali wachukue masomo manne (4) ya taaluma na masomo ya fani moja ya Elimu ya Amali. Masomo ya



Taarifa ya Kamati Final.indd 66 08/05/2023 15:05

taaluma yanayopendekezwa ni Hisabati, Elimu ya Biashara, Kiingereza, na Historia ya Tanzania na Maadili. Aidha, wanafunzi wa mkondo wa Elimu ya Amali wawe huru kuchagua masomo ya ziada ya taaluma kulingana na uwezo na ratiba ya shule husika.

(ix) Aina ya michepuo ya Elimu ya Amali itakayotolewa katika shule mbalimbali izingatie shughuli za uchumi na fursa zilizopo katika maeneo husika. Idadi na aina ya michepuo ipitiwe kila baada ya muda ili kuhakikisha inaendana na matakwa ya wakati.

(x) Shule za sekondari za ufundi zilizopo ziimarishwe na kugeuzwa kuwa vitovu vya kufundishia elimu ya Sekondari ya Hatua ya Chini Mkondo wa Elimu ya Amali katika stadi za kihandisi. Pia, tofauti na shule nyingine za Elimu ya Amali, shule hizi ziruhusiwe kutoa zaidi ya fani mbili za Elimu ya Amali.

(xi) Kuifanya kila shule ya sekondari ya Mkondo wa Elimu ya Amali kuwa wakala wa VETA kutasababisha ongezeko kubwa sana la wanafunzi wa Mamlaka hiyo. Kwa sababu ya ongezeko hilo, VETA na NACTVET ziimarishwe ili ziweze kumudu majukumu ya uthibiti ubora wa elimu ya amali iliyopanuka kwa sababu ya kutolewa pia katika shule za sekondari.

(xii) VETA iendelee kutoa kozi zake zote kwa wahitimu wa ngazi zote za elimu wanaotafuta kupata umahiri katika stadi za amali mahsusi kulingana na matakwa yao na fursa za kiuchumi zilizopo ili kutimiza dhana ya elimu bila ukomo. Pia, VETA itoe mafunzo yatakayowezesha wahitimu kupata vyeti vya ubobezi katika fani mbalimbali za elimu ya amali (*high-level certification in specific vocations*) kulingana na mahitaji ya soko.

(xiii) Ili kuongeza wigo wa fursa za kujiunga na elimu ya juu, idadi ya masomo katika kila tahasusi kwa Kidato cha Tano na Sita isiwe chini ya matatu (3) na isizidi manne (4) kulingana na uwezo na malengo ya mwanafunzi.

(xiv) Wanapohitimu Kidato cha Nne, wanafunzi wa mkondo wa Elimu ya Amali watunukiwe cheti cha kumaliza elimu ya sekondari na cheti cha Umahiri wa Elimu ya Amali kinachotolewa na mamlaka husika.

(xv) Wanafunzi wa mkondo wa Elimu ya Jumla waruhusiwe kuchagua somo la ziada kutoka kwenye fani moja ya Elimu ya Amali.

(xvi) Kutokana na kufanya elimu ya lazima kuishia Kidato cha Nne, mtihani wa kumaliza elimu ya msingi (*Primary School Leaving Examination*) ufutwe na badala yake kuanzishwe upimaji wa kitaifa wa Darasa la Sita (*Standard Six National Assessment*).



Taarifa ya Kamati Final.indd 67 08/05/2023 15:05

(xvii) Kiundwe chombo huru na thabiti cha kusimamia ubora wa elimu ya msingi, sekondari na elimu ya ualimu kama ilivyo kwa elimu ya juu na elimu ya ufundi.

(xviii) Mamlaka husika zitoe ufafanuzi bayana wa malengo ya mikondo ya elimu ya juu ya jumla (*general higher education*), ambayo kwa sasa inasimamiwa na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU), na yale ya mkondo wa elimu ya juu ya ufundi (*technical higher education*) ambayo kwa sasa inasimamiwa na NACTVET. Mamlaka hizo kwa pamoja ziandae vigezo vitakavyohakikisha wahitimu kutoka ngazi moja wanaweza kuendelea na mafunzo katika ngazi nyingine.

## 10.2 Mitaala

(i) Kuboresha Dira na Malengo Makuu ya Elimu ili kukidhi mabadiliko ya Sera na mahitaji ya kitaifa.

(ii) Kuboresha mitaala yote kwa kuongeza maudhui ya kisasa, kuondoa maudhui yaliyopitwa na wakati, na kuondoa kujirudia kwa maudhui katika somo na baina ya masomo.

(iii) Kupunguza wingi wa maudhui katika kila somo ili uwiane na muda wa kufundishia na mahitaji ya taifa kwa kuzingatia mifano bora (*best practices*) kutoka mataifa mbalimbali.

(iv) Kubadilisha namna masomo ya lugha yanavyofundishwa kwa kusisitiza mwanafunzi ajenge umahiri katika lugha yenyewe kabla hajaanza kuitumia katika mawasiliano. Aidha, Kiingereza kianze kufundishwa kuanzia Darasa la Kwanza kwa shule zinazotumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia na Kiswahili kianze kufundishwa kuanzia Darasa la Kwanza kwa shule zinazotumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia.

(v) Kuingiza umahiri wa kuhariri, kukalimani na kutafsiri katika mitaala yote ya masomo ya lugha ili kumwezesha mhitimu kutumia ujuzi huu kumudu maisha yake ya kila siku.

(vi) Kuanzisha masomo mapya chaguzi (*optional subjects*) katika ngazi zote za sekondari kama ilivyoainishwa katika Viambatisho Na. 3, 4 na 7.

(vii) Kuanzisha masomo mapya chaguzi (*optional subjects*) katika elimu ya Sekondari Hatua ya Chini mkondo wa Elimu ya Jumla yanayotoa fursa kwa mwanafunzi kupata ujuzi utakaomwezesha kujiajiri au kuajiriwa kama ilivyoanishwa katika Jedwali Na. 5.

(viii) Kuongeza idadi ya michepuo kutoka minne ya sasa hadi tisa (09). Michepuo



Taarifa ya Kamati Final.indd 68 08/05/2023 15:05

mipya inayopendekezwa ni Sanaa, Lugha, Muziki, Michezo na TEHAMA ili kuwajengea wahitimu uwezo wa kushiriki moja kwa moja katika ulimwengu wa kazi.

(ix) Kuunganisha maudhui ya masomo ya Maarifa ya Jamii na Uraia na Maadili kuwa somo moja la Historia ya Tanzania na Maadili ili kufuta kujirudia kwa maudhui.

(x) Kubadili jina la somo la *Information and Computer Studies* (ICS) kuwa *Computer Science* ili kuakisi maudhui yaliyomo.

(xi) Kuanzisha somo la lazima la *Academic Communication* katika hatua ya Kidato cha Tano na Sita linalotilia mkazo wa kujenga uwezo wa kuwasiliana kitaaluma.

(xii) Kufuta somo la *General Studies* katika hatua ya Kidato cha Tano na Sita na kuchanganya maudhui yake katika somo la Historia ya Tanzania na Maadili ili kupunguza kujirudia kwa maudhui.

(xiii) Ili kuongeza wigo wa fursa za kujiunga na elimu ya juu, inapendekezwa kwamba idadi ya masomo katika kila tahasusi isiwe chini ya matatu na wala isizidi manne kulingana na uwezo na malengo ya mwanafunzi. Aidha, aina ya masomo katika kila tahasusi izingatie malengo ya kitaaluma (*career aspirations and pathways*) ya wahitimu na rasilimali zilizopo shuleni.

(xiv) Mwanafunzi aliyefaulu somo la *Additional Mathematics* akiwa Sekondari Hatua ya Chini asilazimike kusoma somo la *Basic Applied Mathematics* katika Sekondari Hatua ya Juu kwa sababu maudhui yake yanafanana.

(xv) Kufuta masomo ya Uraia na Maadili na *Civics* kwa sababu maudhui yake yameunganishwa katika somo la Historia ya Tanzania.

(xvi) Kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia mbinu zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji. Masuala mtambuka, ikiwemo TEHAMA, yafundishwe kwa kuyachopeka wakati wa vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji katika masomo bebezi kwa kuzingatia uhusiano wa suala mtambuka na somo husika.

(xvii) Kuimarisha upimaji endelevu kwa kutumia zana na mbinu zinazopima nadharia na vitendo. Aidha, mfumo wa upimaji utumie vigezo vinavyotambulika vya upimaji wa maendeleo ya kila siku ya mwanafunzi na tathmini ya mwisho ya kukamilisha ngazi husika kwa kuzingatia mtaala wa ujenzi wa umahiri.

(xviii) Upimaji endelevu upewe uzito wa kutosha na uchangie uzito usiopungua


Taarifa ya Kamati Final.indd 69 08/05/2023 15:05

asilimia 30 ya upimaji wote. Aidha, upimaji wa masomo ya Elimu ya Amali ufanyike kwa kuzingatia sheria na taratibu za NACTVET.

(xix) Kusuka upya somo la Biashara (*Commerce*) ili limfundishe mwanafunzi mbinu na mikakati ya kuanzisha na kuendesha biashara kwa ufanisi. Kwa sababu hiyo jina la somo hilo limebadilishwa kuwa Elimu ya Biashara (*Business Studies*) na litakuwa la lazima kwa wanafunzi wote wa ngazi ya Sekondari Hatua ya Chini.

(xx) Kuyafanya masomo ya *Biology* na *Geography* kuwa chaguzi kwa sababu maudhui yake muhimu yamejumuishwa kwenye masomo ya Sayansi na Jiografia na mazingira katika Elimu ya Msingi.

(xxi) Kupunguza idadi ya masomo ya lazima katika ngazi ya Sekondari Hatua ya Chini kutoka saba (7) hadi sita (6) kama ilivyofafanuliwa kwenye kielelezo Na. 4.

## 10.3 Elimu ya Ualimu

(i) Walimu tarajali wa Awali na Msingi wawe wahitimu wa Kidato cha Sita badala ya Kidato cha Nne na watunukiwe Stashahada baada ya kuhitimu kozi ya miaka miwili (2).

(ii) Kufuta stashahada ya ualimu wa sekondari na kufanya walimu wote wa ngazi hii wawe na shahada ya elimu au stashahada ya uzamili katika elimu. Aidha, vyuo vya ualimu ambavyo kwa sasa vinatoa mafunzo ya stashahada ya ualimu wa sekondari vitumike kama vituo vya kutoa mafunzo endelevu kwa walimu (*continuous professional development*).

(iii) Kuanzisha Astashahada Maalumu ya Elimu kwa ajili ya kuandaa wakufunzi wa karakana (*workshop instructors*) watakaosaidia kuendesha mafunzo kwa vitendo katika karakana/maabara. Astashahada hii itatolewa kwa muda wa miezi sita kwa wahitimu wa stashahada za ufundi sanifu.

(iv) Kushauri vyuo vya elimu ya juu vianzishe programu za fani mbalimbali za elimu ya amali na ualimu kama vile Uhandisi na Ualimu, Sanaa Bunifu na Ualimu, Urembo na Ualimu, Uvuvi na Ualimu na kadhalika. Aidha, uandaaji wa walimu wa Elimu ya Amali na utayarishaji wa miundo mbinu ya kufundishia na kujifunzia vianze mara tu baada ya mapendekezo haya kukubaliwa.

(v) Baada ya kuhitimu, walimu tarajali wafanye kazi chini ya uangalizi (*internship*) kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuimarisha umahiri na



Taarifa ya Kamati Final.indd 70 08/05/2023 15:05

weledi katika fani ya ualimu. Serikali kupitia wizara inayohusika na elimu iandae mwongozo wa namna ya kusimamia mafunzo haya.

(vi) Kuimarisha mitaala ya ualimu kwa kuboresha maudhui na kusisitiza mafunzo ya mbinu za kufundishia, maadili na weledi.

(vii) Kuanzisha somo jipya la lazima linalotilia mkazo kujenga uwezo wa kuwasiliana kitaaluma (*professional communication for teachers*) katika lugha watakayotumia kufundishia.

(viii) Mwalimu tarajali afundishwe kwa kutumia lugha ambayo ataenda kufundishia.

(ix) Serikali iboreshe maslahi ya walimu ili kutoa motisha kwa walimu na kuiongezea hadhi fani ya ualimu. Aidha, Sheria Na. 6 ya mwaka 2018 iliyoanzisha Bodi ya Usajili wa Walimu ambayo ina jukumu la kusimamia maadili na weledi kama ilivyo kwenye tasnia nyingine itekelezwe kikamilifu.

## 10.4 Utekelezaji

(i) Utekelezaji wa mitaala mipya uanze mwaka 2024 kwa makundi ya madarasa kwa kuanzia na darasa la chini kama ifuatavyo: Katika mwaka wa kwanza, mitaala mipya ianzie Darasa la Awali, Darasa la Kwanza, Darasa la Tatu, Kidato cha Kwanza, Kidato cha Tano na mwaka wa Kwanza wa Elimu ya Ualimu.

(ii) Kwa mkondo wa elimu ya amali, utekelezaji uanze mwaka 2025 katika shule chache zilizochaguliwa kimkakati ili kutoa muda wa kutosha wa maandalizi. Kwa mpango huu mzunguko wa utekelezaji wa mitaala mipya utakamilika mwaka 2027 isipokuwa kwa sekondari ya chini elimu ya amali ambapo utakamilika mwaka 2028.

## 10.5 Sheria

Mapendekezo yote yatakayokubaliwa ambayo yanahitaji mabadiliko ya sheria mbalimbali zinazohusu elimu na ustawi wa mtoto yazingatiwe kabla mitaala pendekezwa kutekelezwa.

RASIMU

## Marejeleo


Bikorimana, E. (2020). 25 years of Rwanda Teachers Education reform and development to promote a more resilient economic growth. *Journal of Emerging Technologies and innovative Research (JETIR), 1* (1), pp. 166-180.

Department of Basic Education (n.d.). *Initial Teacher Education*. Republic of South Africa. Available Online at https://www.education.gov.za

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1982). *Mfumo wa Elimu Tanzania 1981-2000. Ripoti ya Maendeleo ya Tume ya Rais ya Elimu*. Juzuu la Pili. Dar es Salaam: Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2002). *Sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 na rekebisho lake Sura ya 353 ya mwaka 2002*. Dar es Salaam: Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2004). *Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (Sheria Kuu) Sura ya 366 ya Mwaka 2004*. Dar es Salaam: Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

Mauritius Institute of Education (2015). *National Curriculum Framework Nine Year Continuous*. Mauritius Institute of Education.

Ministry of Education (2007). *Teacher Development and Management Policy in Rwanda*. Kigali.

Ministry of Education (2018). *National Pre-tertiary Education Curriculum Framework*. Ministry of Education, Republic of Ghana.

Ministry of Education and Culture (1995). *Education and Training Policy*. Dar es Salaam: Ministry of Education and Culture.

Ministry of Education, Science and Technology (2019). *Framework for the Implementation of three year Diploma in Teacher Education for Science and Business Studies*. Dar es Salaam: Tanzania Institute of Education.

Ministry of Education, Science and Technology (2019). *National Curriculum Framework for Basic and Teacher Education*. Tanzania Institute of Education.

Ministry of Science and Technology (1996). *The Technical Education and Training Policy in Tanzania*. Ministry of Science and Technology.

Ministry of Education and Vocational Training (MoEVT) (2014). *Education and Training Policy*. Dar es Salaam: MoEVT.


RASIMU



Taarifa ya Kamati Final.indd 72 08/05/2023 15:05

Nyerere, J. K. (1967). Education for Self-Reliance. Dar es Salaam: Tanzania Government Printer.

Nyerere, J. K. (1988). *Twenty Years of Education for Self-Reliance*. Paper presented at CHAKIWATA Symposium, Moshi, Tanzania.

OECD [Organisation for Economic Co-operation and Development] (2011). *Building a High-quality Teaching Profession: Lessons from around the World*. Paris: OECD Publishing.

OECD [Organisation for Economic Co-operation and Development] (2020). *Education Policy Outlook 2020*: Country Policy Profiles 2020. Paris: OECD Publishing. http://www.oecd.org/education/profiles.htm

OECD [Organisation for Economic Co-operation and Development] (2022). *Education Policy Outlook 2022*: Transforming Pathways for Lifelong Learners. Paris: OECD Publishing. https://doi.org/10.1787/c77c7a97-en.

Republic of Kenya (2019). *Basic Education Curriculum Framework.* Nairobi: Kenya Institute of Curriculum Development.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2019). *Mtaala wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu*. Dar es Salaam: WyEST.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2019). *Taarifa ya Kikaokazi cha Kujadili Uboreshaji wa Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Astashahada*. Dar es Salaam: WyEST.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2019). *Mtaala wa Elimu ya Msingi Darasa la I–VII*. Dar es Salaam: WyEST.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2022). *Ripoti ya Utafiti wa Maoni ya Wadau wa Elimu kuhusu Uboreshaji wa Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu*. Dar es Salaam: WyEST.

Tanzania Institute of Education (2007). *Curriculum for Ordinary Level Secondary Education in Tanzania*. Dar es Salaam: MoEST.

Tume ya Rais ya Elimu (Presidential Commission for Education) (1982). *Ripoti Juu ya Mapendekezo ya Elimu nchini Tanzania*. (Makweta's Report).

United Republic of Tanzania (URT) (2018). *The Tanzania Teachers' Professional Board Act, 2018*. Dar es Salaam.

United Republic of Tanzania (URT) (2021). *Basic Education Statistics in Tanzania (BEST)*. Dar es Salaam: Ministry of Education, Science and Technology.



Taarifa ya Kamati Final.indd 73 08/05/2023 15:05